SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**NMB** yachangia mil. 400/- za matibabu ya kinamama wenye ugonjwa wa fistula

UKURASA 4


Nipashe Spotika

NYOTA 10 WALIOFUNGA HAT-TRICK MECHI YAO YA KWANZA UEFA UK. 12

REKODI 5 ZA GUINNESS ALIZOWEKA RONALDO

ISIKUPITE

UKURASA 11

Nipashe

Jumatatu Septemba 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580716

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Aidai hospitali bil. 1.5/- tuhuma za kumsababishia utasa



UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, na Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), wakimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 400, Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi, kwa ajili ya matibabu ya kinamama wenye fistula. Wapili kulia ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 3

### ACT YATAJA SABABU KUTOSHIRIKI KIKAO NA MSAJILI, JESHI LA POLISI

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakitashiriki kikao kilichopangwa kuvikutanisha vyama vya siasa...

UKURASA WA 4

### SERIKALI YATOA MAELEKEZO UKATILI WANAWAKE KAZINI

SERIKALI imevitaka vyama vya wafanyakazi, vya waajiri na taasisi zote kujitathmini...

UKURASA WA 5

### CHADEMA YATOA MSIMAMO MGOMBEA URAIS MWANAMKE

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeeleza msimamo wake kuhusu kuweka...

# Makamba aanika sababu TANESCO kutojiendesha

**Atoa** maagizo manane kwa mameneja ngazi zote...*Endelea ukurasa 2*

## EWURA yaja na angalizo uchakachuaji gesi kupikia

UKURASA 3

**MICHEZO** MTIFUANO SIMBA, YANGA SASA WAHAMIA LIGI KUU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Makamba aanika sababu TANESCO kutojiendesha

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema kuna sababu nyingi zilizokuwa zinalikwamisha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kujiendesha, mojawapo ni serikali kuingilia uendeshaji pamoja na maamuzi ya kisiasa.

Hivyo, ameahidi kuwa chini ya uongozi mpya wa shirika hilo ulioteuliwa hivi karibuni, hakutakuwa na maamuzi ya kisiasa wala misukumo ya kisiasa katika uendeshaji wa shirika hilo.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye mkutano maalum uliowakutanisha mameneja wa kanda, wilaya, mikoa wa TANESCO, kwa lengo kuu la kutoa dira, mwelekeo mpya wa shirika hilo.

"Sababu iliyokuwa inakwamisha ni uendeshaji wa shirika na uongozi wa shirika. Lakini nataka kukubali na kukiri hata sisi serikali kuna baadhi ya nyakati tuliingilia uendeshaji wa shirika kwa namna ambayo siyo msaada kwa shirika," alisema Makamba na kuongeza:

"Katika mambo mapya serikali kutojiingiza katika uendeshaji wa shirika hili, nawaahidi hakutakuwa na maamuzi ya kisiasa na pressure (misukumo) ya kisiasa katika uendeshaji wa shirika kuanzia sasa. Kuanzia sasa shirika hili ni la kwenu, tumewaletea uongozi mpya, bodi mpya."

**ATOA MAAGIZO**

Kadhalika, Waziri Makamba alitoa maagizo manane kwa mameneja wa kanda, wilaya na mikoa wa TANESCO ambayo ni kuhakikisha shirika hilo linajiendesha kibiashara, kiufanisi, pamoja na kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Pia aliwataka kuhakikisha wanaongeza mapato serikalini, kuwajali wateja na watumishi, kumaliza tatizo la kukatika ovyo kwa umeme, kuwapo kwa bei nafuu ya umeme, pamoja na TANESCO kuwa shirika lenye thamani na kueshimika barani Afrika.

"Siyo ndoto ya alinacha, ni jambo linalowezekana, nyie ndiyo askari wetu wa miguu. TANESCO ndilo shirika lenye makusanyo makubwa kuliko yote nchini, kwa mwaka jana lilikusanya Sh. trilioni 1.8.

"Ndilo shirika linaloajiri watu wengi, ndilo shirika lenye mali nyingi zenye thamani ya Sh. trilioni 13. Linauza bidhaa isiyouzwa na mtu yoyote. Hivyo hakuna sababu ya kusuasua wala kushindwa," alisema Makamba.

Alisema uteuzi uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan wa viongozi wapya wa shirikia hilo unatoa taswira namna serikali inavyotaka kuwapo kwa mapinduzi makubwa kwenye sekta ya umeme.

Alisema nia ya serikali ni kuona TANESCO likijiendesha kwa faida na kuongeza nguvu ya kiuchumi kwa kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza umeme katika nchi za Zambia, Kenya na Malawi.

Makamba alisema: "Shirika hili lilikuwa likiendeshwa pasipo kuwa na ufanisi, kila mtu anapaswa kufahamika kiwango chake cha ufanisi, shirika halitaendeshwa kimzaa, hakutakuwa na uonevu, tunatarajia uadilifu na uchapakazi."

Aliongeza: "Shirika hili ni la kihuduma, lakini tunataka liendeshwe kibiashara hivyo wanaoliendesha wanapaswa kuwa na mtazamo huo, tunataka tupate gawio wakati hakuna manung'uniko ya wafanyakazi," aliongeza.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema miradi mingi ya serikali ipo katika Sekta ya Nishati, kwamba mameneja wa kanda, mikoa na wilaya ndiyo kielelezo cha kuifanikisha.

Alisema zaidi ya Sh. trilioni 2.385 za Wizara ya Nishati zimeelekezwa katika miradi ya maendeleo sawa na asilimia 98.9, huku asilimia moja pekee ikielekezwa katika mambo mengineyo.

Naye Mkurugenzi Mkuu mpya wa TANESCO, Maharage Chande, alisema kitu cha kwanza ataanza na kuwapa motisha wafanyakazi, kuwapa zawadi wanapofanya vizuri pamoja na kuboresha maslahi.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Baraza la nne la Wafanyakazi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), uliofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro. Wakwanza kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru. **PICHA: HESLB**

# Aidai hospitali bil. 1.5/- kwa madai kumsababishia utasa

**Na Hellen Mwango**

FLORAH Lengwana, mkazi wa jijini Arusha, amefungua kesi ya madai Mahakama Kuu jijini Dar es Salaam dhidi ya Hospitali ya Kairuki na daktari wake, akidai fidia ya Sh. bilioni 1.5 kwa madai ya uzembe na uharibifu uliosababishwa wakati akipatiwa matibabu kati ya mwaka 2018 na 2019.

Katika kesi hiyo Lengwana anataka hospitali hiyo kumlipa fidia ya Sh. milioni 800 ya uharibifu uliosababishwa, Sh. milioni 80, malipo ya adhabu, Sh. milioni 700 uharibifu wa jumla na amri nyingine ni hospitali hiyo na daktari kwa uzembe na kumsababishia madhara.

Mlalamikaji, anaituhumu hospitali hiyo na daktari wake kwa pamoja kwa uzembe uliosababisha madhara makubwa yasiyorekebishika ya kuondolewa kizazi na kupoteza tena tumaini au nafasi yoyote ya kushika mimba au kuzaa watoto.

Kesi hiyo inatarajiwa kuanza kusikilizwa ushahidi wa mlalamikaji Oktoba 21, mwaka huu mbele ya Jaji Lilian Itemba.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya pande zote mbili kushindwa kufikia makubaliano kwa njia ya usuluhishi.

Ilidaiwa katika hati ya madai kuwa Julai 2, 2018, wakati hakuwa mgonjwa au kusikia maumivu yoyote, mlalamikaji alikwenda hospitali kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi wa saratani ya kizazi, ambayo hapo awali alikuwa akifanya kawaida kila baada ya miaka mitatu.

Alidai alipofika mapokezi ya hospitali hiyo na baada ya kusajiliwa, mlalamikaji alishauriwa kuwa kabla ya kufanyiwa uchunguzi huo lazima kwanza amuone daktari wa magonjwa ya wanawake, ambaye ilidaiwa alikuwa Dk. George Chugulu kwa kujaza fomu za NHIF ili aweze kuhudumiwa.

Pia, ilidaiwa mlalamikaji alimweleza Dk. Chugulu historia fupi ya kiafya ambayo naye aliagiza afanye vipimo vingine kadhaa, pamoja na Hysterosalpingography (HSG) na suala la uchunguzi wa saratani halikushughulikiwa.

Hati hiyo ya madai iliendelea kueleza badala yake, Dk. Chugulu anadaiwa alimshauri mlalamikaji huyo afanye vipimo vya utasa kabla ya kuruhusiwa kufanya uchunguzi wa Paps Mear.

Mlalamikaji alidai kupitia hati yake ya madai kuwa ushauri wa daktari na jinsi alivyoshughulikia suala lake ulijaa uzembe na usiokubalika.

Katika majibu yao, walalamikiwa wote kwa pamoja wamekanusha madai hayo katika hati yao ya pamoja ya utetezi na wanamtaka mlalamikaji huyo athibitishe madai hayo.

Pia kwa ufafanuzi Dk. Chugulu anapinga kuwa na uhusiano wowote na Hospitali ya Kairuki.

Walalamikiwa wanasema kuwa mlalamikaji alifika hospitalini Julai 2, 2018, akitaka ushauri wa daktari kuhusu malalamiko yake yanayohusiana na kutokuwa na ujauzito kwa zaidi ya miaka sita tangu amzae mtoto wake wa pekee aliyezaliwa baada ya kufanyiwa matibabu tofauti katika hospitali kadhaa.

Wanadai kuwa baada ya kuelezea maisha yake na historia ya matibabu, Daktari Chugulu alishauri kufanya vipimo alivyofanyiwa mlalamikaji, ambavyo vilikuwa muhimu kujua sababu ya shida zake na hatua inayowezekana ya kusaidia katika kutatua shida hiyo.

Walalamikiwa wanadai kuwa hakukuwa na uzembe au kitu chochote kibaya kwa ushauri uliopewa mlalamikaji, ambao aliukubali kwa yeye kusaini fomu za NHIF na kuonyesha utayari wa kufanyiwa vipimo vya matibabu katika maabara na Idara ya Radiolojia ya hospitali hiyo.

## HABARI KITAIFA

# EWURA yaja na angalizo uchakachuaji gesi kupikia

**Na Christina Mwakangale**

KUTOKANA na malalamiko ya baadhi ya watumiaji wa gesi ya kupikia kwamba wanauziwa bidhaa hiyo bila kuwa na ujazo unaostahili, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa maelekezo.

Mamlaka hiyo imewataka wauzaji wa gesi ya kupikia kuzingatia kanuni ya kuwapo kwa mzani kwenye maduka yao ili kumhakikishia mteja uzito wa mtungi unaoendana na ujazo pamoja na bei.

Kadhalika, imewataka wanunuaji wa gesi hiyo kutumia haki yao kuhakikisha wanapofika dukani kupima mtungi kwenye mzani kabla ya kuuziwa.

Pia EWURA imezitaka kampuni zinazouza mitungi hiyo kuhakikishe zinaweka maelezo ya kimaandishi katika kila duka, kuhusu bei ya kila mtungi kulingana na ujazo na uzito sahihi.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu suala hilo baada ya gazeti hili kupokea malalamiko kutoka kwa watumiaji wa gesi ya kupikia hususan majumbani, wakidai ujazo si sahihi kulingana na uzoefu wao katika matumizi ya bidhaa hiyo.

Baadhi ya watumiaji wa gesi ya kupikia majumbani hususan kinamama mkoani Dar es Salaam, wanaeleza kutilia shaka ujazo wa mitungi ya gesi ya kupitia.

Fauzia Abdallah, mkazi wa Buguruni jijini Dar es Slaam, alisema matumizi ya nishati hiyo ni msaada kwake na kumfanya aachane na utumiaji wa mkaa, ambao awali ulisababisha kutumia kati ya Sh. 50,000 hadi 60,000 kwa mwezi.

"Ninaishi mimi, msichana wa kazi na mtoto wangu mdogo ambaye mchana kutwa anashinda shuleni kurudi saa 10 jioni, hivyo mapishi ni vitu vichache tu dada... mwenyewe anayeshinda nyumbani atapika chai, chakula cha mchana na kuandaa mboga za pamoja kwa ajili ya usiku.

"Nikinunua mtungi mdogo wa gesi unaouzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 21,000 ninakaa nao mwezi mmoja hata na nusu. Lakini siku hizi wiki tatu mtungi umeisha, ninagombana na dada kwa sababu gharama zinakuwa kubwa, ndani ya mwezi ninunue gesi mara mbili. Bora nirudi kutumia mkaa kipimo kidogo kwa siku 2,000," alisema Fauzia.

Grace Sawaka, mkazi wa Kinondoni, alisema hivi sasa ameamua kutumia nishati aina mbili tofauti, ikiwamo mkaa na gesi kutokana na matumizi ya gesi kuongezeka licha ya utumiaji kuwa ni uleule.

"Mimi sishindi nyumbani na nyumba nzima wote tunatoka kwenda kujitafutia, tunanunua mtungi wa gesi wa kati unaouzwa kati ya Sh. 48,000 au 50,000 na matumizi yalikuwa ni mwezi au miezi miwili, ajabu sasa mtungi wiki tau umeisha."

Chibulunje, akifafanua zaidi kuhusu suala hilo alisema maduka yaliyo mengi yanayouza gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hawana mzani wa kupima mtungi kabla ya kumuuzia mteja.

"Sheria inavyotaka ni kuupima mtungi, na wenye mzani ni wachache sana labda mawakala wakubwa. Wenye maduka madogo ya bidhaa zingine na ana mitungi yake labda sita au 10 hawana mzani. Na wanunuzi wakubwa wapo mtaani kusiko na wakala.

"Mitungi mingi inayouzwa kwenye maduka madogo unaweza ukaunyanyua mtungi kwa mkono tu, mteja anapima kwa mkono ulio mzito ndio anauchukua na kulipia. Utaratibu wa kuweka mzani uwapo kila duka, kwa sababu mtaani mawakala wakubwa hawapo.

# ACT yataja sababu kutoshiriki kikao na Msajili, Jeshi la Polisi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakitashiriki kikao kilichopangwa kuvikutanisha vyama vya siasa na Jeshi la Polisi Oktoba 21, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwenye vyombo vya habari jana na Katibu wa Habari, Uenezi, Uhusiano na Umma wa chama hicho, Salim Bimani, wamefikia uamuzi huo baada ya kutafakari kwa kina.

"Tumepata taarifa kupitia vyombo vya habari kuwa kikao cha Jeshi la Polisi na vyama vya siasa kilichoitishwa na Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa kimepangwa kufanyika Oktoba 21, mwaka huu. Baada ya kutafakari kwa kina, ACT-Wazalendo tumeamua kuwa hatutashiriki kikao hicho," alisema Bimani.

Alisema sababu za chama hicho kuamua kutoshiriki kikao hicho ni pamoja na ratiba ya kikao baina ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi kuingiliana na ratiba na vikao vya viongozi wakuu wa chama hicho.

"Oktoba 21 hadi 22, mwaka huu, viongozi wakuu wa chama chetu watakuwa kwenye mkutano mkuu wa kitaifa wa haki, amani na maridhiano ulioitishwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania(TCD). Mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Bimani.

Alisema sababu nyingine iliyochangia chama hicho kufikia uamuzi huo ni kutopatiwa mrejesho wa barua yao waliyoituma kwa Msajili wa vyama ya kuomba kikao hicho kimshirikishe Waziri wa Mambo ya Ndani.

"Baada ya msajili wa vyama vya siasa nchini kutangaza kikao na vyama hivyo, ACT-Wazalendo kupitia kwa Kiongozi wa chama Zitto Kabwe, kilimwandikia barua kuwa kikao hicho kimjumuishe Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye ndiye mwenye dhamana ya kisiasa na Jeshi la Polisi. Hadi sasa hatujapata mrejesho wa suala hilo na mwelekeo ni kuwa kikao hicho kitakuwa cha polisi na vyama vya siasa pekee," alisema Bimani.

Pia chama hicho kinadai kwamba sababu nyingine ya kuamua kutoshiriki kikao hicho ni kutokana na matamshi ambayo kimekuwa kikiyasikia kwa baadhi ya viongozi wanaotarajiwa kukutana nao, kuonyesha kwamba huenda kikao hicho kikatumika kubinya zaidi shughuli za kisiasa nchini.

"Matamshi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, baada ya kikao chake na Msajili wa Vyama vya Siasa hayaonyeshi nia njema ya kikao hicho," alisema Bimani.

"Kauli yake kuwa nchini Tanzania hakuna shida kuhusu mikutano ya nje na kwamba tatizo lipo kwenye mikutano ya ndani na inabidi sheria iwekwe sawa, ni dalili ya wazi kuwa kikao hicho kinaweza kutumika kubinya zaidi shughuli za kisiasa nchini."

Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, alitangaza kufanyika kwa vikao hivyo vikiwa na lengo la kumaliza misuguano ambayo imekuwa ikijitokeza baina ya Jeshi la Polisi na vyama hivyo na tayari kikao cha awali kimefanyika kati ya ofisi ya Msajili na Jeshi hilo na Oktoba 21 itakuwa ni zamu ya vyama hivyo la Jeshi la Polisi.


**Air Tanzania**
The Wings of Kilimanjaro

## TRAINING INSTITUTE

## EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is implementing its five years Corporate Strategic Plan (2017/2018-2020-2021) which includes the network expansion in local, regional and international destinations as well as improvement of its internal operations and human capital management. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the position of Senior Human Resources Officer in Human Resources and Administration Unit.

**1. POSITION: Senior Human Resource Officer (Engagement & Employees Welfare) 1 (ATCL HQ)**

**2. REPORTING LINE:** Head of Human Resource and Administration

**3. QUALIFICATIONS:**

The following are qualifications for aspired candidates: -

- Must have Bachelor Degree in Human Resources Management/Public Administration/Political Science and Public administration or Degree in Commerce/Business Administration Majoring in Human Resource Management or its equivalent from recognized University/Institution.
- Must have at least 5 years' experience in service as Human Resource Officer in a competitive business environment.
- A proven background in provision of counselling services in a multicultural and multidisciplinary business environment is an added advantage
- A formal training in counselling at least to certificate level is an added advantage

**4. COMPETENCIES:**

- High levels of empathy
- Mental health, counseling methods and techniques.
- Organizational and time-management skills
- Excellent communication, interpersonal and facilitation skills
- Critical thinking
- Problem-solving and flexibility
- Strong ethical standards

**5. DUTIES AND RESPONSIBILITIES.**

The holder of the position will perform the following duties and responsibilities:

- Develop and oversee implementation of cost-effective staff engagement, team building and change management strategies;
- Develop, oversee and monitor the implementation of the work-life balance guidelines
- To oversee the implementation of leadership development programmes
- Develop and oversee implementation of strategies that will attract employees to open up about their mental health
- Coordinate interdepartmental and intradepartmental communication strategies
- Listen to employees' concerns, seeking ways to address them
- Initiate and implement interdepartmental, departmental, sections and units stress management activities that will also to promote team work
- Plan, implement and manage the overall Talent Acquisition Strategy
- Prepare periodic reports
- Perform any other official duties that may be assigned by supervisor

**6. TERMS AND CONDITIONS:**

Five (5) years contract with remuneration and fringe benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme

**7. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**8. CLOSING DATES:**

Applicants should consider the following closing dates for this post as follows:

**Within Fourteen (14) days from the first date of this announcement**

**Applicants who previously applied for similar position may re-apply**

**The application letters should be directed to the following address: -**

**Managing Director and CEO, Air Tanzania Company Limited,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM**
**25th September, 2021**




**PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com**
**website:www.airtanzania.com**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akiongea na Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Taifa ya Biashara, Elvis Ndunguru (kushoto), wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya Nne ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yanayoendelea Mjini Geita. Benki hiyo imepokea na kuanza kufanyia kazi kwa kutenga shilingi bilioni 20 maelekezo ya Waziri Mkuu ya kukopesha wachimbaji wadogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa maelekezo ukatili wanawake kazini

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imevitaka vyama vya wafanyakazi, vya waajiri na taasisi zote kujitathmini upya kwa kuhakikisha vinaweka dhamira ya dhati ya kutokomeza ukatili wa wanawake mahala pa kazi ambao umekithiri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi na Ajira), Jenister Mhagama, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua kongamano la wadau kuhusu ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake maeneo ya kazi.

Kongamano hilo ambalo limeandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) likiwa na kauli mbiu isemayo, 'Uwajibikaji kutokomeza udhalilishaji mahali pakazi' lilikwenda sambamba kwa kufanyika mkutano mkuu wa mwaka.

Waziri Mhagama alisema vitendo vya ukatili wa wanawake mahali pa kazi vinaacha madhara na maumivu makubwa kwa wahanga na jamii inayowazunguka.

"Ninatoa wito kwa wafanyakazi, vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri na taasisi zote kuwa mstari wa mbele kuonyesha kwamba vimedhamiria kukomesha ukatili wa wanawake mahala pa kazi.

"Hatuwezi kuwa na taasisi hizi imara halafu bado ukatili unaendelea, turudi tukajitathmini wajibu wetu ndani ya vyama hivi kama tunautekeleza vizuri. Lengo la vyama vya wafanyakazi ni kutetea maslahi na ustawi wa wafanyakazi maeneo ya kazi."

Kwa mujibu wa Mhagama, kama ukatili unaendelea, lazima warudi kuangalia sera na sheria ndani ya vyama hivyo kwa hali iliyopo sasa, kama zinatekeleza au wanatakiwa kufanya mabadiliko yake.

Alisema kwa upande wa sheria za kazi wizara yake ipo tayari kukaa navyo, ili kufanya marekebisho na kupata maeneo ambayo yanaweza kusaidia kufanya vita hiyo iwe rahisi. "Ipo mikataba ambayo tumeridhia na mingine ambayo bado hatujaridhia hatuna budi kufanya kazi ya kina kuangalia uridhiaji wa mikataba hiyo, utengenezaji sheria zinazohusu mikataba hiyo ili ziendane na mazingira, mila na desturi tulizonazo," alisema. Waziri huyo alipongeza hatua iliyofikiwa na WiLAF Tanzania ya kupinga matukio hayo na kuwaeleza kuwa wanastahili kupongezwa na yeye yupo tayari kushirikiana nao.

"Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inatambua na imeamua kuhakikisha inawalinda wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia na tutafanyakazi hiyo kwa nguvu zetu zote. "Kwenye hili kongamano mmesema ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wenu unaosema wanawake na ajira na lengo ikiwa ni kuboresha mazingira mazuri ili wanawake waweze kushiriki katika shughuli za uchumi na viwanda ninawapongeza."

Alisema mradi huo unaendana na dhana nzima ya Rais Samia ambaye ameamua kuwa balozi wa wanawake kwa kutekeleza kwa vitendo usawa wa kijinsia kwa kuona umuhimu wa wanawake kushiriki katika ujenzi wa uchumi.

Alisema Rais Samia amevunja miiko iliyokuwapo tangu uhuru kwa kufanya uteuzi kwenye nafasi ambazo hazijawahi kushikwa na mwanamke akitolea mfano uteuzi wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stegomena Tx.

Mwenyekiti wa WiLDAF, Monica Mhoja, alisema lengo la kongamano hilo ni kujadili ukatili na udhalilishaji wa wanawake katika sekta ya kazi na ajira.

Alisema lengo lingine ni kupendekeza mbinu na kuandaa mpango mkakati wa pamoja katika kuondoa matatizo yaliyopo sehemu za kazi.

Edmund Moshy kutoka Mwakilishi wa Shirika la Kazi Ulimwenguni (ILO), aliiomba serikali kuridhia na kuupitisha mkataba wa 190 unyanyasaji mahali pa kazi ambapo mpaka sasa nchi sita tu ndiyo zimeuridhia.

# NMB yachangia mil. 400/- matibabu wenye fistula

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Benki ya NMB kwa kuwa mshirika mkubwa wa serikali katika kuleta maendeleo kwenye sekta mbalimbali hasa elimu na afya, baada kuchangia Sh. milioni 400 za matibabu ya wenye ugonjwa wa fistula.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa marathon iliyopewa jina la Mwendo wa Upendo kuchangia matibabu ya wagonjwa wa fistula iliyoandaliwa na benki hiyo kwa kushirikiana na Hospitali ya CCBRT jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema amekuwa akifuatilia shughuli za Benki ya NMB na kubaini mwaka mzima wanakuwa karibu na jamii kufanya jambo hili au lile kwa lengo la kuondoa changamoto za kielimu au afya.

"NMB wamekuwa watu wa kusaidia jamii mwaka mzima, nimewashuhudia mara kwa mara wakisaidia madawati, vifaa vya kujifunzia, mabati kwa ajili ya kuezeka vyumba vya madarasa, wakati mwingine wanasaidia vifaa tiba.

"Huu ni mfano mzuri unaofaa kuigwa na taasisi nyingine za kifedha, serikali yenu inawaunga mkono katika hili na niwape salamu za Rais Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango wapo na nyinyi," alisema Majaliwa.

Alibainisha kuwa ugonjwa wa fistula unawatesa sana kinamama, hivyo NMB kufikiria kuchangisha fedha kupitia Marathon ya Mwendo wa Upendo ni jambo la kipekee ambalo haliwezi kusahauliwa kirahisi kwa kila atakayeguswa.

"Ninasema wazi NMB nyinyi ni wabunifu, njia mnayoitumia kurudisha fadhila kwa jamii ni ya kipekee, ninawaahidi serikali itashirikiana nanyi kuwaletea maendeleo Watanzania," alisema Majaliwa.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema mbio za mwaka huu zimeleta hamasa kubwa na kuonyesha Watanzania wapo tayari kusaidia jamii kupitia michezo, hivyo NMB imeamua badala ya kutumia miaka minne kutafuta shilingi bilioni moja waliyopanga kuipata ili kusaidia wagonjwa wa fistula, fedha hizo watazitafuta ndani ya mwaka mmoja.

"Tulikuwa na nia ya kukusanya shilingi milioni 250 kila mwaka, lakini leo tumevuka lengo tumekusanya shilingi milioni 400, nakuahidi ndugu mgeni rasmi tutakusanya shilingi bilioni moja ndani ya mwaka mmoja badala ya minne tuliyoahidi awali," alisema Mhede.

Alibainisha: "Hiki unachokiona hapa watu kujitokeza kwa wingi na kuchangia matibabu ya fistula kinatokana na utendaji kazi wetu unaowavutia wengi, ndiyo maana faida tunayoipata hatusiti kuirudisha kwa jamii kama sehemu ya shukurani zetu kwao."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema wameamua kuja na mpango huo baada ya kuona namna wanawake wanavyoteswa na ugonjwa wa fistula, gharama ni kubwa na wengi wanashindwa kukidhi.

"Fistula ni hali inayosababishwa na uzazi pingamizi ambapo kwa mujibu wa takwimu za UNFPA, Tanzania hivi sasa kuna wanawake zaidi ya 10,000 wenye fistula na takribani wagonjwa wapya 3,000 huongezeka kila mwaka, lakini wagonjwa 1,300 pekee ndio wanaopata matibabu," alisema Zaipuna na kuongeza:

"Gharama kubwa za matibabu ya tatizo hili ndio kisababishi kikubwa kwa wanawake wengi kutopata matibabu ya fistula. Tumetaarifiwa kwamba gharama ya tiba kwa mwanamke mmoja ni takribani shilingi milioni nne, gharama ambayo ni kubwa kwa Mtanzania wa kipato cha kawaida.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO**
**MADAI YA PESA**
**NO: 96/2021**
**POPOTE ULIPO**

**NDUGU: ROBERTSON MICHAEL SIMBAGIJE**
**WA: TEMEKE**

**MADAI YA PESA NO. 10,300,000/=**

**MDAI: EDWARD EPIMACK LASWAI**
**MDAIWA: ROBERTSON MICHAEL SIMBAGIJE**

Mtajwa hapo juu unaamriwa na Mhakama hii kuja kusikiliza shauri lililotajwa hapo juu siku ya **IJUMAA tarehe 29/9/2021 saa 2:30 asubuhi** bila kukosa na kama hukuhudhuria shauri hili litasikilizwa upande mmoja.
Amri hii imetolewa kwa amri yangu leo **tarehe 15/9/2021.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO
DAR ES SALAAM

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO**
**DAR ES SALAAM**

116478302



**KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI**

**GERSHON RUBEN HOTAY** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki aina ya **FEKONI 125 namba ya usajili MC 678 CKB,Chasis No. LDAPAJOB3KGBO6592 , Engine No. 157FMI-2 19FO6592, Taarifa ya Polisi DOD/CHA/RB/424281/2021.Pikipiki aina ya FEKONI 125 namba ya usajili MC 584CLU,Chasis No. LDAPAJOB4KGBO7587, Engine No.157FMI-2 19FO7587,Taarifa ya Polisi DOD/CHA/RB/424291/2021.Pikipiki aina ya SINOLAY 15018 namba ya usajili MC 285CSK,Chasis No LD3PCK6J8L2012743 ,Engine No.SR162FMJ 20092743 Taarifa ya Polisi DOD/CHA/RB/424268/2021.Pikipiki aina ya SINOLAY 125,namba ya usajili MC160 CLN,Chasis No. LD3PCJ6JSK2010554 ,Engine No.SR156FMI 19110554 Taarifa ya Polisi DOD/CHA/RB/424274/2021.**
**Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.**

116478902



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MIKESE**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.14/2021**

Ombi la **ALLY KIKA ALLY** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **MWANAIDI SAID CHASINYA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 26/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe 06/09/2021**

MAHAKAMA YA MWANZO
MIKESE

116478402



**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA**
**YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO.157/2019**
**DICKSON A.MWAIKAGA::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**

**1.ANYIMIKE W.MBWAGHA:::::::::::::::MDAIWA**
**2.MUSSA NKEMBO BAHO:::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA :**
**ANYIMIKE W.MBWAGHA,**
Fahamu kwamba **DICKSON ANYOSISYE MWAIKAGA** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe **05/10/2021 saa 2:30** asubuhi mbele ya **Mh.T.Munzerere** Mwenyekiti wa Baraza .Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya with huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka :** Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo **tarehe 15/09/2021.**

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**

116478702

HABARI KITAIFA

## Hukumu kesi dawa za kulevya Okt. 29

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imepanga kutoa hukumu ya wafanyabiashara tisa akiwamo Mwanaidi Mfungo (59), maarufu kama Mama Leila, wanaokabiliwa na mashtaka ya kuingiza nchini dawa za kulevya aina ya heroine na cocaine kilo tano.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Jamhuri kuita mashahidi wanane na kuwasilisha vielelezo 21 dhidi ya washtakiwa na utetezi kuita mashahidi tisa.

Kesi hiyo imesikilizwa mbele ya Jaji Isaya Arufani na mawakili wa pande zote mbili kuwasilisha hoja za majumuisho ya mwisho, Jamhuri wakiomba mahakama iwaone wana hatia na utetezi wakiomba iwaone hawana hatia na iwaachie huru.

Jaji Arufani alisema baada ya kusikiliza ushahidi na majumuisho ya mwisho mahakama yake itatoa hukumu Oktoba 29, mwaka huu.

Washtakiwa wengine ni Sara Munuo (47) Anthony Karanja (42), Ben Ngare (36), Almas Said, Yahaya Ibrahim, Aisha Kungwi na Rajabu Mzombe ambao walisomewa mashtaka yao kwa mara ya kwanza mwaka 2011 mpaka sasa ni miaka 10, wako mahabusu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa, Juni mosi, 2011, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikamatwa wakiingiza dawa za kulevya aina ya cocaine.

Washtakiwa walikana mashtaka hayo.



Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa Daraja la JPM (Kigongo–Busisi), Yang, akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (kushoto), wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa mita 3,200 ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2024, jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHADEMA yatoa msimamo mgombea urais mwanamke

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeeleza msimamo wake kuhusu kuweka mgombea mwanamke katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kikisema hiyo siyo ajenda muhimu kwa wananchi na kutaka ziangaliwe sifa za mgombea bila kujali jinsia yake.

Akizungumza na gazeti hili katika makao makuu ya chama hicho, Dar es Salaam juzi, Naibu Katibu Mkuu Benson Kigaila ,alisema kwa sasa chama hicho kinaendelea kujiimarisha katika maeneo mbalimbali kupitia mkakati waliouita CHADEMAa Digital, na kwamba itakapofika muda wa kusimamisha wagombea wataangalia sifa.

"Hiyo siyo ajenda muhimu mbona ADC mwaka 2020 walisimamisha mwanamke, kwani nani alisema kwamba kuna ajenda na kuna vyama vingi vimeshasimamisha wagombea wanawake mara nyingi tu... mbona hatujasema ,Anna Mgwhira aligombea kupitia ACT-Wazalendo alikuwa mwanamke?" alihoji Kigaila.

"Tutasimamisha mtu kwa uwezo wake na siyo kwa jinsia yake ,na huyo mwanamke hatakiwi kuungwa mkono, kwa sababu ya jinsia yake anatakiwa kuungwa mkono kwa uwezo wake " alifafanua.

Akizungumzia kuhusu suala la rufani ya waliokuwa viongozi katika Baraza la Wanawake (BAWACHA) katika chama hicho Halima Mdee na wenzake, Kigaila alisema bado chombo cha kufikia uamuzi wa suala hilo ambalo ni baraza kuu la chama hicho halijakaa kufanya uamuzi wa rufani yao.

"Baraza Kuu halijikaa kusikiliza rufani yao, litakaa na haitakuwa siri itatangazwa," alisema

Halima Mdee na wenzake 18 walitimuliwa uanachama na uongozi wa chama hicho mwaka jana, baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum kwa kile kilichodaiwa ni kukiuka msimamo wa chama hicho.

Hata hivyo walikata rufani kwa kile walichodai kuwa mchakato wa kuwavua uanachama haukuwa halali, ingawa mpaka sasa rufani bado haijasikilizwa huku wakiendelea na nafasi zao za ubunge.

Kuhusu hali ya kisiasa na uongozi ya chama hicho kutokana na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, kushitakiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na hivyo kukosekana katika uongozi wa chama hicho Kigaila alisema pamoja na kuendelea kupambana na kesi mahakamani lakini hakuna kilichoharibika kwa kuwa wapo viongozi wengine.

**Imeandikwa na Enock Charles , Pauline Lugaziya na Leyla Joho**

## Watiwa mbaroni kwa madai kutotumia vitabu vya madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani kahama, Mkoa wa Shinyanga imewakamata wamiliki 10 wa mialo ya kuchenjua dhahabu katika migodi midogo ya Mwime Gold Mine na Bumbiti Gold Rush kwa madai ya kutokutumia vitabu vya kutunza kumbukumbu za uchenjuaji wa madini.

Hali hiyo imetajwa kuchangia serikali kupoteza mapato yake kwa sababu madini mengi yanayochenjuliwa katika mialo hiyo yanauzwa kwa njia ya magendo, huku mengine yakitoroshwa na kwenda kusikojulikana.

Pia imemwagiza kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini Kahama, Jeremia Hango, kufanya ukaguzi wa vitabu vya kumbukumbu za utunzaji wa taarifa za madini katika mialo yote inayohusika na uchenjuaji wa dhahabu ili kukomesha tabia hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwakamata wamiliki hao alipofanya ziara ya kushtukiza akiwa na Kamati yake ya ulinzi na usalama katika machimbo ya Mwime Gold Mine na kubaini udanganyifu huo unaofanywa na baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara ambao sio waadilifu.

"Nimeagiza wamiliki hawa 10 watozwe faini kwa mujibu wa sheria za madini na wengine watakaobainika kukiuka sheria kwa makusudi... hatutatoa nafasi ya kulipa faini na badala yake tutawapeleka mahakamani kwa makosa ya uhujumu uchumi," alisema Kiswaga.

"Ukiangalia hali ya uuzaji wa madini kwenye masoko yetu imeshuka, lakini uzalishaji bado upo juu, mwezi uliopita masoko yetu yaliuza dhahabu yenye kilogramu 25, ambayo imezalishwa na wachimbaji wadogo, lakini kwa sasa wameanza kutumia njia zisizo rasmi kutorosha madini tena."

Kiswaga aliwataka wachimbaji na wamiliki wa mialo kutojihusisha na vitendo vya utoroshaji wa madini kwa sababu serikali imeweka mitego kila sehemu kubaini wanatorosha madini.

Nae Hango alisema, atatekeleza agizo hilo na atakuwa akilifanya mara kwa mara ili kuendelea kuwakumbusha wajibu wao wamiliki wa mialo namna ya kutunza kumbukumbu na kuuza madini yao katika masoko yaliyotengwa na serikali.

Aidha alisema, wametoa vitabu maalum vya kutunza kumbukumbu za taarifa za uzalishaji kwenye mialo hadi dhahabu inaposafirishwa kwenda sokoni, lakini baadhi yao wanajaza taarifa za uongo na kwamba watakaowabaini watawafungulia mashtaka badala ya kuwatoza faini.

Mwenyekiti wa wachimbaji wa dhahabu Wilaya ya Kahama, Joseph Nalimi, aliiomba serikali kuwapatia vifaa na elimu ya utambuzi wa miamba ili kuepuka uchimbaji wa kuhamahama, ambao unachangia kuharibu mazingira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Karibu Ligi Kuu 2021/22, waamuzi tendeni haki

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2021/22, linafunguliwa rasmi leo katika viwanja vitatu baada ya juzi kupigwa mechi ya Ngao ya Jamii iliyowakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga, ikiwa maalum kwa ajili ya kuukaribisha msimu mpya.

Kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu kuanza, huchezwa mechi ya Ngao ya Jamii, ambayo humkutanisha bingwa wa Ligi Kuu na wa Kombe la Shirikisho (FA Cup), hivyo miamba hiyo miwili ilikutana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na Yanga kuibuka kidedea baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 likifungwa na Fiston Mayele.

Simba ilipata nafasi hiyo ya kucheza mechi ya Ngao ya Jamii baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho, hivyo kucheza na Yanga ambayo fursa hiyo iliiangukia kwao kutokana na kufika fainali ya FA Cup msimu uliomalizika.

Hivyo, pazia la Ligi Kuu 2021/22, leo litafunguliwa kwa kucheza mechi tatu katika viwanja tofauti ambapo mjini Morogoro, Mtibwa Sugar itaikaribisha Mbeya Kwanza FC mchezo ukipigwa Uwanja wa Jamhuri wakati Namungo FC ikiwa mwenyeji wa Geita Gold FC katika Dimba la Ilulu mkoani Lindi na Azam FC ikikabiliana na Coastal Union ugenini katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. Ligi hiyo itaendelea kesho kwa kupigwa michezo mingine mitatu ambapo Dodoma Jiji itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati Mbeya City ikiwa mwenyeji wa Tanzania Prisons katika Dimba la Sokoine jijini Mbeya huku mabingwa wa ligi hiyo, Simba wakiwa wageni wa Biashara United katika Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Michezo ya kwanza ya raundi hiyo ya kwanza kwa kila timu itakamilika Jumatano kwa Polisi Tanzania FC kuikaribisha KMC FC katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi na Kagera Sugar kuwa wenyeji wa Yanga katika Dimba la Kaitaba mjini Bukoba.

Kwa ujumla msimu huu unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa zaidi ya misimu iliyopita hasa kutokana na kiasi kikubwa cha udhamini kilichowekwa kwenye haki za matangazo ya televisheni baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Kampuni ya Azam Media Limited Mei, mwaka huu kuingia mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 225.6 kwa kipindi cha miaka 10.

Katika mkataba huo ambao mgao wa fedha kwa kila klabu unatakiwa kuelekezwa kwenye mishahara ya wachezaji, kutakuwa na bonasi kuanzia klabu itakayotwaa ubingwa hadi itakayoburuza mkia, ambapo bingwa atazawadiwa Sh. milioni 500, mshindi wa pili milioni 250, watatu milioni 225, wa nne milioni 200 na zitakwenda zikipungua hadi timu ya mwisho na zile zitakazocheza mechi ya mtoano zikilamba milioni 20 kila moja.

Kiasi hicho ni mbali ya fedha zitakazotolewa na wadhamini wenza pamoja mdhamini mkuu wa ligi hiyo ambaye kwa mujibu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), mazungumzo yamefikia pazuri na anatarajiwa kutangazwa hivi karibuni.

Hivyo, ongezeko hilo la fungu ni wazi haitakuwa ligi ya lelemama, kwani tayari timu zote zimeonyesha kudhamiria kufanya vizuri kutokana na aina ya usajili uliofanywa kwa klabu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo msimu huu. Kwa mantiki hiyo, hatutarajii kuona waamuzi wakiwa chanzo cha malalamiko kutoka kwa baadhi ya klabu kwa kutozitendea haki kwa kufinyanga sheria 17 zinazoongoza mchezo huo duniani.

Tunataka kuona kila timu ikipata matokeo kutokana na uwezo wake uwanjani na si kubebwa na waamuzi kutokana na mapenzi au ushabiki wao kwa baadhi ya klabu, kupewa rushwa ama vinginevyo. Waamuzi hawana budi kutambua klabu hizi zimewekeza jasho, nguvu kubwa na fedha katika suala zima la uendeshaji, hivyo Nipashe tunataka haki ikitendeka ndani na nje ya uwanja na si tu kutendeka bali ionekane ikitendeka kweli na ifahamike mapema kwamba hatutafumbia macho hata kidogo kwa mwamuzi ama yeyote yule mwenye dhamira mbaya ya kutaka kufinyanga matokeo kwa nia yake ovu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mabeki wa pembeni Simba chanzo kikuu kipigo Yanga

**NI** kama tayari Yanga wameshaizoea Simba, wameshaisoma udhaifu wao ambao wapinzani wao hawajashtukia, au mpaka sasa hawajui jinsi gani ya kuupatia dawa.

Kwa mara nyingine, Yanga iliondoka na ushindi wa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuwaacha wanachama na mashabiki wa Simba wakiwa hawaamini kilichotokea.

Kwa miaka ya hivi karibuni wanachama na mashabiki wa Simba wanaamini kuwa timu yao ni bora zaidi kuliko Yanga, inawezekana ikawa hivyo, lakini kwa mwaka huu wa 2021, Yanga imepata ushindi mara tatu dhidi ya Simba. Kwa mwaka huu, zimeshakutana mara nne, huku zikitarajiwa kukutana tena Desemba 11 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu. Zilianza kukutana Januari 13, kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar, ikiwa ni fainali ya Kombe la Mapinduzi, na Yanga kulitwaa kombe hilo kwa kuifunga Simba kwenye matuta, baada ya dakika 90 kwenda sare ya bila kufungana. Yanga ilishinda kwa mikwaju 4-3 ya penalti.

Mechi ya pili ilikuwa Julai 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliyokuwa ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu wa 2020/21. Kwenye mechi hiyo, Yanga ilishinda kwa bao 1-0, lililofungwa na Zawadi Mauya. Mara ya tatu ni kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA, Julai 25, Uwanja wa Tanganyika, Simba ikishinda bao 1-0. Mechi ya Jumamosi ilikuwa ni ya nne kwa watani hao msimu huu na ya tatu kwa Yanga kuibuka na ushindi.

Kuna baadhi ya mashabiki wanadai kuwa pengo la Clatous Chama na Luis Miquissone limeonekana na ndilo lililosababisha Simba ifungwe.

Hata hivyo, ukiangalia hata Luis na Chama kabla hawajaondoka, Simba imekuwa ikipata ugumu kuifunga Yanga na hata mechi ya Julai 3 ikifungwa bao 1-0 walikuwapo. Ikumbukwe hata mechi ya Machi 8, mwaka jana, Bernard Morrison akiwa Yanga, Simba ililala bao 1-0, Chama na Luis walikuwapo pia.

Ni ukweli mchungu pia kinachoonekana kuwahangaisha Simba kwenye mechi dhidi ya Yanga ni mabeki wao wa pembeni.

Tayari Yanga wameshagundua kuwa Shomari Kapombe na Mohamed Hussein wanapenda kupanda mbele, lakini kwa siku za karibuni ama wamekuwa wazito kurudi kukaba au hawako kwenye viwango vyao vya kawaida.

Hata sajili za Yanga zinaonekana zaidi kulenga pembeni kwa mawinga wenye mbio, ili kuwahangaisha mabeki wa wapinzani wao.

Ndiyo maana walimsajili Tuisila Kisinda ambaye alikuwa akiwahangaisha sana mabeki wa pembeni wa timu hiyo, hata alipouzwa haraka walimsajili Jesus Moloko kwa kazi hiyo hiyo.

Bado wakamsajili Djuma Shaaban wakiamini atasaidia kumnyanyasa Tshabalala kama alivyofanya wakati akiwa AS Vita Club kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa. Na kweli, hilo Yanga wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Ndiyo maana ukiangalia mpira mingi ya Yanga ilikuwa ikipitia pembeni na kuwa ni ya hatari kubwa. Ukiiangalia sasa Simba ina udhaifu mno kwa mabeki Tshabalala na Kapombe hasa kwenye kukaba kwa siku za karibuni.

Ikumbukwe kuwa Tshabalala kiasili si mzuri sana kukaba, lakini ni mzuri kupandisha mashambulizi, lakini kadri muda unavyozidi kwenda upande wake unaonekana unapitika kirahisi zaidi.

Kapombe naye tangu msimu uliopita hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida, kwa sasa amepungua uwezo na ana makosa mengi sana.Kwa maana hiyo wamekuwa wakiwapa tabu sana kina Thadeo Lwanga, Paschal Wawa, Joash Onyango na hata alipoingia Kennedy Juma, walilazimika kuwasaidia wenzao, na hata wakifanya hivyo, wanakuwa wakiacha mapengo kati.

Kama Yanga wasingekuwa waoga, kuiogopa Simba na kuamua kushambulia muda wote, kwenye mechi hizi zote wangekuwa wanafunga mabao mengi.

Ukiangalia mechi ya Jumamosi, Yanga walikuwa hawashambulii muda mwingi, lakini wanapoamua kushambulia, wanakuwa hatari zaidi na hawazuiliki hasa wakipitia pembeni. Ashukuriwe Wawa na Kennedy ambao walifanya kazi kubwa mno kuwazuia mastraika wa Yanga, na pia mawinga wao ambao Tshabalala na Kapombe walishindwa kabisa kuwazuia. Niliona Kocha Mkuu, Didier Gomes akiamua kumtoa Tshabalala na kumwingiza Israel Mwenda ambaye alikuja angalau kuleta uhai na kutuliza mashambulizi.

Hii ni kengele ya hatari kwa benchi ya ufundi la Simba kuwa Yanga wameshagundua udhaifu wa timu yao upo kwenye beki wa kulia na kushoto. Na ndiko wanakotumia zaidi, Simba inakwenda kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Jwaneng Galaxy. Wakati tatizo la ufungaji likitafutiwa ufumbuzi, lakini kuna tatizo mama la kuruhusu mashambulizi kirahisi pembeni. Ikumbukwe hata TP Mazembe bao lao lilipitia pembeni. Udhaifu wa Kapombe ulimlazimu Aishi Manula atoke golini. Inawezekana timu za nje, zisigundue sana udhaifu huo wa Simba kwa sasa au wakachelewa kuugundua, lakini Yanga ndiyo imekuwa ikiutumia hata kama wakiambiwa kesho wanarudiana na Simba.

Desemba 11 timu hizo zinakutana tena, kama Gomes hatotafuta dawa ya Tshabalala na Kapombe, basi wala haitoshangaza Simba ikafungwa kwa mara nyingine tena mechi hiyo.

## SMZ yasisitiza falsafa ya uchumi wa kidigitali, bluu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imebainisha dhamira yake ya kuhakikisha wananchi wanakuza uchumi wa kisasa unaoendana na falsafa ya uchumi wa kidijitali na uchumi wa bluu.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar Amoul Hamil, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akikabidhi kituo cha Kompyuta kwa Umma (Tele-Center) kwa Shule ya Sekondari Tumbatu kilichojengwa kwa udhamini wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa lengo la kutoa huduma za TEHAMA kwa walimu, wanafunzi na jamii ya kisiwa kidogo cha Tumbatu kilichopo umbali mfupi kutoka kisiwa cha Unguja.

"Matarajio yetu kama serikali ni kwamba sasa tunakwenda kutekeleza dhamira yetu ya dhati, ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza dira zetu za maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora na matumizi mapana ya suala zima la TEHAMA," aliongeza.

Alibainisha kwamba wizara yake itakachofanya ni kuhakikisha inaweka mikakati ya kuhakikisha shule nyingi zaidi na jamii ambazo hazijafikiwa na TEHAMA zinapata huduma hiyo muhimu katika ukuzaji wa uchumi wa kisasa.

Amesema kituo hicho cha TEHAMA ambacho kimedhaminiwa na TCRA ni cha sita miongoni mwa vituo vilivyopatiwa miundombinu wezeshi ya TEHAMA chini ya mpango wa TCRA wa fungu la TEHAMA (ICT-pack) ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma za mawasiliano hasa maeneo ambayo hayajafikiwa, kikitarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 3,000.

Akizungumzia kwa niaba ya Mkurugenzi TCRA wakati wa kukabidhi vifaa vya kituo hicho, Mkuu wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Esuvatie Masinga, alibainisha kuwa lengo la TCRA ni kuhakikisha huduma za TEHAMA zinakuwa jumuishi na kuwafikia wananchi wengi zaidi kote nchini.

"TCRA Ofisi ya Zanzibar katika kutekeleza mpango huu wa kutoa kwa jamii vifaa vya TEHAMA tumeamua kwa awamu hii kujikita kwenye visiwa ndani ya visiwa kwa upande wa hapa Unguja tuna vituo viwili tumevifungua; hiki ni kituo cha sita na tuna mpango kwamba mwaka ujao wa fedha tutaomba fedha ili twende kisiwa cha Kojani na maeneo mengine ya Zanzibar, lengo likiwa kufikisha huduma za Mawasiliano na TEHAMA kwa jamii kubwa zaidi," alifafanua Masinga. Masinga akisaini hati ya makabidhiano ya Kituo cha TEHAMA katika kisiwa cha Tumbatu, Zanzibar kilichofadhiliwa na TCRA kuwezesha upatikanaji wa huduma za TEHAMA katika elimu na jamii.

Wanufaika wa mradi huo walielezea furaha yao kwa kujengewa kituo cha TEHAMA kwa kuwa kitarahisisha upatikanaji wa huduma za elimu na kuwawezesha wananchi wa Tumbatu kuwasiliana kwa urahisi na kuendana na ukuaji wa TEHAMA.

Akiwasilisha salamu za wakazi wa Tumbatu na menejimenti ya shule, Mkuu wa shule hiyo alieleza kuwa kituo hicho sit u kitasaidia ujifunzishaji miongoni mwa wanafunzi na kitawezesha upatikanaji wa huduma za TEHAMA miongoni mwa wanafunzi wa shule mbili za sekondari zilizopo kwenye kisiwa hicho.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Aie Holding Limited ya nchini Israel, Avi Postelnik, akizungumza na waandishi wa habari jijini hivi karibuni kuhusu kampuni hiyo kutaka kuja kuwekeza miradi mbalimbali hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## M'biashara adai kuvunjiwa duka, mali zake kuporwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

MFANYABIASHARA Ezekia Mwashemele wa jijini hapa amemwomba Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitilia Mkumbo, kuingilia uvunjwaji wa duka lake na kuchukua bidhaa mbalimbali hali iliyomsababishia hasara ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema alivunjiwa duka lake lililokuwa Mtaa wa Viwandani, Kata ya Mwakibete jijini Mbeya, Septemba 9, mwaka huu na kwamba ameshatoa taarifa polisi na wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Viwandani, Kata ya Mwakibete, Robert Mwambela, alisema uvunjaji wa duka hilo ulikuwa na upungufu kwa kuwa mhusika hakupewa barua ya 'order' iliyotoka Baraza la Ardhi na Nyumba.

"Sisi kama uongozi wa mtaa tarehe 9/9/2021 ilikuja order toka Baraza la Ardhi la Wilaya na watu watatu toka kampuni ya Pamoja Auction Mart Comp.Ltd, order hiyo haikuwafikia walengwa wa vyumba hivyo vya biashara, tulipohoji wakasema hawajapatikana tukaona kuna upungufu," alisema mtendaji huyo katika barua aliyomwandikia Msajili wa Wilaya Mahakama Kuu ambayo gazeti hili imeiona.

Mfanyabiashara huyo alisema uvunjaji huo ulifanywa na watu wanne na Mbunge mstaafu wa Jimbo la Rungwe kupitia CCM, Sauli Henry Amon, anadaiwa kushirikisha vijana wake kutekeleza kazi hiyo.

Mwashemele ambaye alikuwa amepanga katika jengo la Royal Zambezi tangu mwaka 2014, alidai watu hao kwa kushirikiana na mbunge huyo baada ya kuvunja duka hilo walichukua bidhaa mbalimbali yakiwamo matairi ya magari mapya zaidi ya 200, rimu, betri, tube na oil za magari.

"Kinachonishangaza wavunjaji wanajinasibu kuwa hawashindwi polisi wala mahakamani hivyo nimeshuhudia maana walifunga duka bila order yoyote ile inayo nihusu mimi kila ninapoenda nikitaja jina la aliyefunga hakuna mwitikio wowote wala hatua inayo chukuliwa," alisema.

Alisema sababu za kuvunjiwa duka lake ni kuuzwa kwa jengo hilo na kisheria wahusika walitakiwa kuwajulisha wapangaji kwa kuwapatia barua au mikataba ya kutoka mmliki wa kwanza kwenda kwa mmiliki wa pili ambaye ni S.H. Amon Enterprises Limited, lakini hawakufanya hivyo na badala yake walifunga duka lake kwa zaidi ya miaka minne na kisha kulivunja mwezi huu na kuondoka na vitu vilivyomo ndani.

Alidai kuingizwa kwenye mgogoro huo tangu Februari 23, 2018, na kwamba S.H. Amoni (Sauli) andaiwa kuituma mtu (anamtaja) akiwa na kundi la watu kufunga duka lake wakati akiwa safarini na kijana aliyekuwa akiuza duka hilo alitolewa nje na kufunga kwa kufuri na kuondoka nayo.

Kwa mujibu wa nyaraka ambazo gazeti hili imezione ni kwamba mgogoro huo ulikuwa ni kati ya Sauli (mbunge mstaafu) na mmiliki wa jengo hilo Ndele Mwandoje ambaye alibadili jina na sasa anaitwa Amani Nuru Mtiwauzima.

Mwashemele alisema kutokana na biashara yake kukwama muda mrefu, amekuwa akipata usumbufu kutoka kwa watu wa benki ambako alikopa hela Sh. milioni 80 kwa ajili kuendesha biashara hiyo na sasa wanatishia kuipiga mnada nyumba yake.

Alisema suala hili amelifuatilia katika vyombo mbalimbali, lakini bado hajapata msaada na kumwomba waziri mwenye dhamana na biashara amsaidie ili aendelee kufanya biashara yake.

Mfanyabiashara huyo alisema tangu mgogoro huo uanze hali yake kimaisha imeyumba na kushindwa kusomesha watoto wake.

Akizungumza tuhuma hiyo, mbunge huyo mstaafu Sauli alisema mfanyabiashara huyo hawezi kuvunjiwa duka lake bila kuwapo sababu na kwamba hiyo ilikuwa ni 'order' ya mahakama na kumshauri kama hajatendewa haki aende mahakamani.

## Wanaoishi kando ya migodi hatarini kupata magonjwa ya saratani

**Na Richard Makore,** MWANZA

WANANCHI wanaoishi na kufanya kazi katika maeneo ya migodi mikoa ya Kanda ya Ziwa wapo hatarini kukumbwa na magonjwa ya saratani na kuzaa watoto wenye ulemavu kutokana na kunywa maji yenye madini ya zebaki.

Madini hayo yanatumiwa kuoshea mchanga wenye dhahabu ili kupata dhahabu kamili kazi inayodaiwa kufanyika kiholela katika ukanda huo yanapotikana madini ya dhahabu.

Akizungumza katika semina ya siku moja kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya migodi, Mkaguzi wa mazingira Kanda ya Ziwa, kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Festo Mligo, alisema tatizo hilo ni kubwa na kunahitajika nguvu za ziada katika kutoa elimu.

Alisema maeneo yanapochimbwa madini ya dhahabu kuna uhaba wa maji na wananchi wanalazimika kutumia maji yenye madini ya zebaki.

Aliongeza kuwa maji hayo yakitumiwa na binadamu pamoja na wanyama yana madhara ya kiafya ambayo hayawezi kuonekana sasa hadi baada ya miaka mingi.

Aidha, alisema binadamu akila nyama ama samaki aliyekunywa maji hayo anaweza kupata madhara ya kiafya na Kanda ya Ziwa ipo katika hatari zaidi.

Aliongeza kuwa kanda hiyo inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa kansa na kwamba sababu mojawapo inayotajwa ni kutokana na kutumia maji yenye madini ya zebaki. Wakizungumza katika semina hiyo, baadhi ya wajumbe walisema wananchi wanaozunguka maeneo hayo wanatumia maji ya visima vya asili ambayo sio salama kwa kuwa yameingiliana na madini ya zebaki inayotumika kuoshea mchanga wa dhahabu. Walisema baadhi ya wananchi wanatakaa kutumia maji ya visima vilivyochimbwa na serikali ambavyo maji yake yamepimwa kwa madai kwamba hayana ladhi na badla yake kuendelea kutumia ya visima vya asili.

Kwa upande wake, Meneja wa mradi wa Tanzania Women Empowerment in Action (TAWEA), ambao wanafanya utafiti kuhusu tatizo la maji katika maeneo ya migodi, Alpha Ntayomba alisema tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ni kubwa.

Alisema maeneo ya migodi yakiwamo ya Nyarugusu na Rwamgasa mkoani Geita, upatikanaji wa majisafi na salama bado sio mzuri na wachimbaji wanatumia maji ya mito na ziwa kuchenjulia dhahabu kwa kutumia zebaki.

Aliomba jamii pamoja na vyombo vya habari kuendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya kutumia maji hayo yaliyochanganyikana na zebaki ili kunusuru afya zao.

HABARI KITAIFA

# Sababu uwekezaji viwanda kukwama yatajwa

**Elizabeth Zaya na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, amesema sababu kubwa inayokwamisha uwekezaji kwenye viwanda ni tija ndogo kwenye mazao yanayozalishwa nchini.

Alitoa kauli hiyo jijini Dodoma wakati akizindua kituo cha usambazaji teknolojia za kilimo cha Nzuguni, Kanda ya Kati.

"Tunajua tatizo linalotukabili kwenye sekta ya kilimo na siyo fumbo kwa sababu tunajua tanatakiwa tufanye nini ili kubadilisha kilimo. Wawekezaji wanasita kuja kuwekeza kwenye viwanda kwa sababu mazao ya kilimo yana tija ndogo," alisema Profesa Mkenda.

"Ukimwambia awekeze kiwanda kwa ajili ya alizeti, anakuuliza je uzalishaji wake ukoje, siyo naweka kiwanda halafu mwisho wa siku nakosa malighafi. Kwa hiyo bado tuna tatizo kubwa la kuongeza tija kwenye mazao yetu." Aliisema Tanzania imekwama kuuza baadhi ya mazao nje ya nchi kutokana na kukosa tija kwa mazao hayo na hata pale walipopata soko la kufanya hivyo.

"Kwa mfano zao la muhogo, tumeshindwa kuuza nje ya nchi kwa sababu halina tija, uzalishaji wake bado siyo wa kuridhisha. Na siyo hilo tu karibu mazao yote bado kuna tatizo kubwa ambalo bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuondoka hapa tulipo," alisema Profesa Mkenda.

Alisema kazi kubwa inayotakiwa kufanyika kwa sasa kuinua sekta hiyo ya kilimo ni kuongeza nguvu katika kutumia utafiti kwenye sekta hiyo, kuzalisha mbegu bora pamoja na kuimarisha shughuli za ugani.

Alisema Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imefanya kazi kubwa ya kitafiti kwa ajili ya kuinua sekta hiyo na kwamba ni vyema wakulima nao wakatumia utafiti huo kwenye shughuli zao ili kuboresha sekta hiyo ya kilimo ilete tija.

"Na tunaamini kwamba wakulima wakitumia tafiti hizi za TARI kwenye kilimo, watakuwa wanazalisha mazao mengi, bei itakuwa chini, lakini wakulima bado watapata kipato, hakuna atakaye umia si mlaji wala mkulima, lakini kwa sasa kwa mfano tunalia mafuta ya alizeti au chakula fulani kimepanda, hii ni kwa sababu mazao yetu hayana tija," alisema Profesa Mkenda.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Tanzania, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema wamejipanga kuhakikisha utafiti wao unasaidia sekta hiyo ya kilimo.

Alisema kituo hicho kitakuwa kinatumika kutoa huduma mwaka mzima za elimu kwa wakulima, maofisa ugani na huduma mbalimbali.



Msanii wa kizazi kipya, Zuwena Mohammed maarufu Shilole, akiwaelimisha wakazi wa Dar es Salaam kuhusu kampeni inayoendeshwa na kampuni Vodacom 'Kimbiza na 4G ya Ukweli' iliyofanyika mwishoni mwa wiki Manzese jijini Dar es Salaam. Kampeni hiyo ina lengo la kuifahamisha jamii kuhusu kasi na uhakika wa mtandao wa Vodacom. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aonya utupaji wa chupa za maji

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ametoa onyo kwa watu wote wenye tabia ya kutupa taka ovyo iliwamo chupa za maji.

Jafo alitoa onyo hilo jana jijini Dar es Salaam katika hotuba yake alipoalikwa na Jumuiya ya Isimailia kushuhudia namna ambavyo jumuiya hiyo inavyounga mkono juhudi za serikali katika kutunza na kusafisha mazingira.

Usafishaji wa mazingira jana ulifanywa na jumuiya hiyo katika Shule ya Msingi Muhimbili, Waziri Jafo akiwa miongoni mwa washiriki wa shughuli hiyo.

Jafo alisema serikali inathamini michango ya wadau mbalimbali katika utunzaji wa mazingira na kuahidi serikali kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha huku akikisisitiza Watanzania kujenga utamaduni wa kutunza mazingira.

"Ninaomba Mkuu wa Wilaya pamoja na viongozi wengine kuweka utaratibu mzuri wa kuhifadhi taka.

Kwa hiyo, ninatoa onyo kwa watu wote wenye tabia ya kutupa taka ovyo kama chupa za maji, ndugu zangu jukumu la utunzaji wa mazingira ni letu sote, waziri huyo alisisitiza.

Waziri Jafo aliipongeza Jumuiya ya Ismailia kwa jitihada ambazo imefanya katika kuunga mkono dhamira ya serikali kwenye utunzaji wa mazingira.

"Kama mnavyojua Rais wetu mpendwa, Mama Samia alipokuwa akihutubia Marekani, ameeleza vipaumbele kabambe vitakavyotumika katika kuendeleza utunzaji wa mazingira.

"Kwa hiyo, katika hili pia niwapongeze sana Jumuiya ya Ismailia pamoja na Aga Khan Development Network kwa kitendo cha kuunga mkono juhudi za serikali katika kusafisha mazingira na kupanda miti.

Alisema dunia kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo hakuna budi ya kila mmoja angalau kwa kila familia kupanda miti mitatu kwenye maeneo yao.

Jafo alitoa wito kwa wadau mbalimbali kujitokeza ili kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika suala la utunzaji wa mazingira kama inavyofanya jumuiya hiyo.

"Kwa kweli hii jumuiya imenikosha, imeniongezea siku za kuishi. Kwa kweli sikutegemea kama nitakuta maandalizi makubwa kama haya, unapokuwa kiongozi halafu ukaona wadau wanaunga mkono jitihada za kile unachokifanya inatia raha sana. Kwa hiyo, niwashukuru sana wanajumuiya na Mungu awabariki," Jafo alisifu.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Muhimbili, Jovitha Mushi, aliishukuru jumuiya kwa kuzuru katika shule hiyo na kueleza kufurahishwa na kitendo hicho.

"Mimi kama mwalimu mkuu katika shule hii, nimefurahi sana kutembelewa na jumuiya hii, kwa kweli leo tumefanya usafi shule nzima, tumepanda miti, lakini pia watoto wamepewa elimu ya kutosha juu ya utunzaji wa mazingira ambayo ninaamini baadaye watakuja kuwa mabolozi wazuri katika utunzaji wa mazingira kama amabvyo serikali inatarajia," alishukuru.

Rais wa Jumuiya hiyo, Amin Lakhani, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika mambo mengine mengi na kuahidi kilichofanyika katika Shule ya Msingi Muhimbili ni kama ufunguzi wa kuendelea kufanya hivyo.

## Wawekezaji sekta ya afya waitwa kuwekeza

**Na Julieth Mkireri**

MBUNGE wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli, ametoa wito kwa wawekezaji wa huduma za kijamii kufika kuwekeza katika Kata ya Bonyokwa, ili wananchi waweze kupata huduma karibu.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa hospitali binafsi ya Harmony Memorial Polyclinic iliyojengwa Bonyokwa Darajani, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

Alimpongeza mwekezaji huyo katika huduma za afya kwa kujenga hospitali hiyo eneo ambalo lina uhitaji.

"Nampongeza sana mwekezaji huyu kwa kuona uhitaji mkubwa kwenye kata hii mpya ambayo ina mahitaji mengi ya huduma za kijamii, niwaalike na wengine waje wawekeze kwani kwasasa huduma nyingi zipo nje ya kata hii," alisema.

Alisema serikali inajitahidi kuongeza vituo vya afya na hospitali zingine katika maeneo mbalimbali ikiwamo kata ya Bongokwa na wanapotokea wawekezaji wanaisaidia kuondoa kero kwa wananchi.

Aliomba uongozi wa hospitali hiyo kuhudumia wananchi kwa gharama nafuu na si kibiashara ili waweze kumudu gharama zitakazowekwa.

Akizungumzia kero ya ubovu wa miundombinu ya barabara, alisema ataenda kufuatilia kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Bonyokwa hadi Kimara ambayo tayari ilishatengewa fedha za ujenzi na serikali.

Awali, akisoma taarifa ya ufunguzi, Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Juliana Mmari, alisema ina madaktari bingwa wa wanawake na watoto, mifupa, wauguzi na wahudumu wa maabara.

Juliana alisema mwishoni mwa mwaka huu wanatarajia kukamilisha chumba cha huduma za dharura na mapema 2022 wataanza kutoa huduma ya wanawake wajawazito.

Alibainisha kuwa hospitali hiyo imetoa ajira kwa vijana 26 kutoka wilaya ya Ilala wakiwamo vijana wasio na taaluma ya utabibu wakifanya usafi na ulinzi.

# Watoto wenye mahitaji maalum kujengewa bweni

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema serikali itapeleka Sh. milioni 80 katika Shule ya Msingi Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya watoto wenye mahitaji maalum.

Waziri Ummy alibainisha hayo alipokuwa katika ziara ya siku moja kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Chalinze ambapo alikagua ujenzi wa madarasa, kuweka jiwe la msingi Bwilingu na kukagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chalinze. Alitoa ahadi hiyo baada ya kupokea ombi kutoka kwa Mbunge wa Chalinze, Ridhiwan Kikwete, kuhusiana na adha wanayopata wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mbali ya fedha hizo, Waziri Ummy pia alisema serikali itatoa Sh. milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule hiyo.

Akiwa katika shule hiyo aliwahakikishia wananchi kuwa hakutakuwa na chaguo la pili kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022, kwani serikali inapambana kuhakikisha uhaba wa vyumba uliopo unakwisha na watakaochaguliwa wote watapata nafasi.

Alisema serikali itatoa Sh. milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Msolwa kuwezesha idadi ya wanafunzi wanaokadiriwa kufaulu waweze kupata nafasi katika shule za sekondari.

"Niwatoe hofu pia katika hili la elimu bure kuna watu wana nia mbovu na kutaka kuleta taharuki, elimu bure itaendelea katika kipindi chote," alisema.

Aidha Waziri Ummy akiweka jiwe la msingi katika Soko la Bwilingu lililojengwa na halmashauri hiyo, aliwaagiza wakurugenzi kuiga mfano wa halmashauri hiyo namna inavyotumia fedha inazopatiwa na serikali na za mapato ya ndani.

Pia aliwaagiza wakurugenzi wote wanapojenga majengo wazingatie maelekezo ya kuweka miundombinu ya watu wenye ulemavu.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema ujenzi wa soko la Bwilingu ni kati ya miradi ambayo ameikagua hivi karibuni ambayo itawawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika sehemu salama.

Kunenge pia aliruhusu wafanyabiashara kufanya shughuli zao saa 24 kutokana na kukua kwa mji wa Chalinze na huduma kuhitajika muda wote.

Ridhiwan alimshukuru Ummy kutembelea halmashauri hiyo na serikali kuendelea kutatua kero za wananchi.



Meneja wa Maendeleo ya Uchumi wa Jamii wa Songas, Nicodemus Chipakapaka (kulia), akikabidhi madawati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 14 kwa Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ally, katika Shule ya Sekondari Mwinyi wilayani Mkuranga. Hadi sasa, Songas imetoa madawati 1,850 kwa shule za mkoa wa Pwani. Wengine ni Mwalimu Mkuu wa Sekondari Mwinyi, Martin Chuwa, Ofisa Elimu Mkuranga, Benjamin Majoya (aliyevaa miwani) na wanafunzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Wengi Geita wajitokeza urasimishaji wa biashara

**Na Felix Andrew**

WANANCHI mkoani Geita wameendelea kumiminika katika banda la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika maonyesho ya nne ya teknolojia ya uwekezaji kwenye sekta ya madini yanayofanyika katika viwanja vya Bombambili mkoani Geita.

Akizungumza baada ya kupata cheti cha usajili wa jina la biashara, mjasiriamali anayezalisha viungo vya chakula Halima Chembemoyo, alisema amekuwa akitumia jina la biashara bila ya kusajili na baada ya kufika banda la wakala kusajili ikabainika kuwa tayari jina hilo limeshasajiliwa na mtu mwingine, hivyo kulazimika kutumia jina lingine.

"Nimelazimika kubadilisha jina langu la biashara ambalo limezoeleka na wateja kutokana na ukweli kwamba nilikuwa nalitumia bila ya kulisajili ninawasihi wajasiriamali wezangu ambao hawajarasimisha biashara zao kutumia fursa iliyopo kwa kufika banda la BRELA na kupatiwa huduma ya papo kwa papo," alifafanua Halima.

Mjasiriamali wa maziwa ya mtindi, Joseph Manoni, akielezea kufurahishwa kwake na huduma za wakala, alisema elimu iliyotolewa ndiyo iliyomhamasisha na kufika katika banda hilo kusajili jina la biashara. Alisema wamekuwa wakikatishwa tamaa huko mitaani kutokana na uvumi kuwa kuna urasimu, lakini baada ya kufika katika banda la BRELA kupata elimu na kupatiwa usaidizi wa kusajili ameridhika na huduma mzuri. Kwa upande wake Ofisa Leseni kutoka BRELA, Yusuph Nakapala, alisema kwa sasa huduma za usajili zimerahisishwa kutokana na maombi yote ya usajili kufanyika kwa njia ya mtandao, hivyo mdau halazimiki kufika katika ofisi zao.

Alisema BRELA inaposhiriki katika maonyesho mbalimbali hutoa usaidizi kwa wadau wanaopata changamoto ya kusajili kwa njia ya mtandao.

Aliongeza kuwa wakala itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari mbalimbali ili uelewa wa pamoja kuhusu usajili uongezeka na hatimaye kupunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Katika maonyesho haya ya siku 10 yanayoendelea mkoani Geita mbali na kutoa huduma za papo kwa papo za usajili, BRELA imetumia fursa ya maonyesho hayo kutoa elimu kwa wajasiriamali mbalimbali waliofika katika maonyesho hayo.

Elimu hii imetolewa katika banda la BRELA, Clinic ya biashara ambayo imejumuisha taasisi mbambali na kuratibiwa na Mamlaka ya Biashara Tanzania(Tantrade) na katika makongamano yaliyoandaliwa na wadhamini wakuu wa maonesho haya Geita Gold Mines na Benki ya NBC.

## Airtel: Tutaendeleza kuwekeza upanuzi wa mtandao vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania imeahidi kuendelea kuwekeza kwenye upanuzi wa mtandao ili kuwapa wateja wake huduma bora hasa kwa maeneo ya vijijini.

Hayo yamesemwa na Meneja Mauzo Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Boniface Mango mwishoni mwa wiki wakati kampuni hiyo ikizindua duka jipya la Airtel Money Branch wilayani humo.

Mango alisema Airtel Tanzania iko kwenye mkakati wa muda mrefu wa kuboresha huduma kwa lengo la kuwafikia Watanzania na hasa walio kwenye maeneo ya vijijini.

"Tunaelewa ni kwa kiasi ngani wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini wanapata changamoto na hasa kwenye sekta ya mawasiliano. Sisi Airtel tumejitolea kuhakikisha kuwa changamoto hizo zote zinapewa ufumbuzi," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kulitambua hilo, kampuni ya Airtel imebadilisha minara yake ya mawasiliano kwenye Wilaya ya Masasi kwenda kwenye Mfumo wa 4G, hivyo kuwapa wananchi wa Masasi uhuru wa mawasiliano. 'Huduma ya Airtel 4G inakuja na teknolojia ya kisasa pamoja na intaneti yenye kazi sana.

"Nawaomba wananchi wabadilishe laini zao kwenda kwenye Mfumo wa 4G ili waendelee kufaidi huduma hii," Mango alisema.

Aliongeza kuwa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za Airtel kwa urahisi na unafuu, kampuni hiyo imefungua maduka ya Airtel Money Branches zaidi ya sita kwenye wilaya yote ya Masasi ili wananchi waweza kupata huduma kwa urahisi na sehemu moja.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Masasi kwenye uzinduzi huo, Efrosina Chikojo, aliwashukuru Airtel kwa jitahada zake za kuleta huduma karibu na wananchi.

"Kampuni ya mawasiliano ya Airtel Tanzania hiko kwenye mkakati wa kuboresha huduma zake ili ziendelee kuwafikia Watanzania hasa kwa maeneo ya vijijini. Kwa hapa wilaya yetu ya Masasi wametumifikia na kwa leo wamewasha minara yao ya 4G pamoja na kufungua maduka mapya ya Airtel Money Branches," alisema Chikojo.

Chikojo aliongeza: "Kwa kampuni kubwa kama Airtel kuleta uwekezaji wake kwenye wilaya yetu hii bila ya kuombwa ni kitu cha kutia moyo na kupongeza. Sisi kama viongozi wa mkoa tunatoa ahadi ya kulinda uwekezaji huu ule uwe na tija kwa wananchi wetu."

# Makandarasi watakiwa kuripoti TAKUKURU wanaowaomba rushwa

**Na Joseph Mwendapole, aliyekuwa** MWANZA

MAKANDARASI nchini wametakiwa kutoa taarifa kwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kuhusu watu wanaowaomba rushwa wakati wa mchakato wa zabuni za miradi ya ujenzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki mkoani Mwanza na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi Consolata Ngimbwa, wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo.

Alisema makandarasi hawapaswi kutoa rushwa wala kushawishi wengine kupokea rushwa kutoka kwao na kwamba iwapo watafanya kazi kwa weledi na maadili rushwa haitakuwa na nafasi kwenye shughuli zao za ujenzi.

"Tukikubali kubadilika wote tutaibadilisha na kuiboresha sekta ya ukandarasi hapa nchini hivyo nawasisitiza mjiepushe kabisa na vitendo vya kutoa na kupokea rushwa," alisema.

Aliwataka makandarasi kushirikiana kupitia ubia kama njia ya kuwawezesha makandarasi wazalendo kupata fursa ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi.

Alisema kutimiza masharti ya miradi mikubwa ni vigumu kwa makandarasi wengi wanapokuwa mmoja mmoja, lakini kwa mfumo wa ubia wanaweza kuyatimiza masharti hayo na kushinda zabuni za miradi mikubwa.

Aliwataka makandarasi kuwa na chama kimoja kitakachokuwa sauti yao kwani sekta hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo haziwezi kutatuliwa kwa urahisi bila kuwa na umoja wenye nguvu.

Naye Naibu Msajili wa CRB anayeshughulikia Utafiti na Maendeleo, Mhandisi David Jere, alisema mafunzo hayo yamehudhuriwa na washiriki 92 wa aina na madaraja mbalimbali kutoka Kanda ya Ziwa na mikoa mingine nchini.

Alisema mafunzo hayo ya usimamizi wa fedha yalilenga kuwasaidia makandarasi kuwa na uelewa wa usimamizi wa rasilimali fedha hususan taarifa za mizania au balance sheet.

Alisema washiriki wa mafunzo hayo wamejifunza masuala ya kodi hususan namna nzuri ya kutunza kumbukumbu ili kuepuka kodi zisizostahili au faini kama adhabu kwa kukiuka misingi muhimu ya uandaaji wa mahesabu ya fedha za kampuni.

Injinia Jere alisema mafunzo hayo ni endelevu na mengine yanatarajiwa kufanyika kwa nyakati tofauti kwenye mikoa ya Iringa, Dar es Salaam na Dodoma.




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule (katikati), akishuhudia ubadilishanaji nyaraka kati ya Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Salman Karmal (kushoto) na Katibu wa Chama cha Wachimbaji Wadogo mkoani Geita (GEREMA), Golden Hainga, baaada ya kutia saini makubaliano ya awali ya kushirikiana wakati wa maonyesho ya madini mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ashtukia hujuma kwenye pembejeo

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Khadija Ally, ameiomba serikali iruhusu kila wilaya ijitafutie pembejeo yenyewe na kuachana na wasambazaji.

Alisema wasambaji hawafikishi pembejeo kwa wakati na hali hiyo inachangia kuwapo kwa kikwazo kwa wakulima wa korosho.

Khadija aliyasema hayo katika kikao cha wadau wa korosho katika Mkoa wa Pwani ambapo mwenyekiti wa kikao, alikuwa Mkuu wa Mkoa huo, Abubakari Kunenge.

Khadija alisema ucheleweshwaji wa pembejeo una changamoto kutokana na pembejeo kutokufika kwa wakati.

"Ikiwezekana kila wilaya isimamie masuala ya pembejeo ili ijitafutie yenyewe," alisema na kuongeza kuwa katika usambazaji pembejeo kuna hujuma kubwa ambazo ni za makusudi.

Alisema pembejeo wakati wa msimu zinakuja kidogo na hizifiki kwa wakati, lakini msimu wa korosho ikiisha ndipo zinapoonekana zikiwa nyingi.

Kwa upande wake, Kunenge naye alionyesha kushangazwa na taarifa za pembejeo na mbolea katika taarifa zilizochapishwa na kugawiwa kwa wadau wa korosho kuzisoma.

Alisema taarifa hizo zinaleta utata kutokana na pembejeo na mbolea kutolewa kwa wakulima mmkoa wa Pwani.

"Mbona hamjaonyesha katika taarifa yenu pembejeo na mbolea kiasi kilichotolewa ikiwamo na idadi ya mikorosho iliyopo Pwani," alisema.

Alisema taarifa hiyo, inatakiwa kuwa imejitoshleza na isije kuleta shida na kwamba inatakiwa ionyesha idadi ya mikorosho iliyopo Pwani na pembejeo pamoja na mbolea zilikuwa kiasi gani na mgao wake ulipelekwaje kwa halmashauri zote.

# TADB yajitosa vita ya corona

**Na Beatrice Moses**

KATIKA kuhakikisha afya ya wafanyakazi na wadau wake zinaimarika sambamba na kujenga uchumi imara wa taifa, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imeratibu na kutoa elimu ya Uviko -19 pamoja utoaji wa chanjo kwa wadau mbalimbali.

Mbali na wadau wamo pia wakiwamo wafanyakazi wa benki hiyo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa zoezi hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema benki hiyo inaunga mkono juhudi za serikali kupambana na Uviko-19, jambo ambalo limeisukuma benki yake kushirikiana na JKCI kuratibu zoezi hilo kutoa fursa kwa wadau wake kupata elimu na chanjo sahihi ili kulinda nguvu kazi kwenye sekta ya kilimo ambayo imeajiri takribani asilimia 60% ya Watanzania wote.

"Leo tumepata wasaa mzuri wa kuendesha zoezi hili, lakini lengo hasa ni kuona elimu kuhusu janga hili la Covid-19 inawafikia wadau wengi na hata huduma ya kuchanja wanaipata hapahapa tena kwa wakati ili kuokoa nguvu kazi hii kubwa kwa taifa," alisema Nyabundege.

Aliongeza: "TADB inatekeleza malengo ya serikali ya kuanzisha chanjo tembezi ambayo itaongeza idadi ja vituo vya chanjo kutoka vituo 550 hadi vituo 6,784 jambo ambalo linatoa fursa wafanyakazi na familia zao kupata huduma hiyo kwenye makao makuu ya ofisi hizo bila gharama zozote."

Aidha, Nyabundege aliwahimiza wadau wa sekta ya kilimo nchini kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vilivyoainishwa nchi nzima ili waweze kujikinga na athari za ugonjwa huo ikiwamo kupoteza maisha.

"Kwa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), inasemekana mpaka sasa watu takribani 4,697,099 wamepoteza maisha kutokana na athari za ugonjwa huu, hivyo basi kwa umuhimu mkubwa niwaombe Watanzania wenzangu kushiriki kikamilifu kupata chanjo ili tuondokane na hatari ya kupoteza maisha utakapopata ugojnwa huu," alisema Nyabundege.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alizipongeza TADB na JKCI kwa kuratibu zoezi hilo na kuwataka wadau mbalimbali nchini kuondoa dhana potofu juu ya chanjo ya ugonjwa huo.

Alisisitiza kuwa maendeleo yoyote katika taifa lolote yanaendana na uwapo wa nguvukazi yenye afya bora, hivyo wajitokeze kwa wingi kupata chanjo kwa faida ya familia yao na hata taifa.

Naye Mkurugenzi wa Kurugenzi wa Magonjwa ya Moyo kutoka (JKCI), Dk. Tatizo Waane, aliwahamasisha watu kujitokeza kuchanja kwa kuwa chanjo hiyo ni sawa tu na chanjo zingine ambazo zinatolewa kwa lengo la kudhibiti athari kubwa ya ugonjwa huo.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 27, 2021

Nipashe

Spotika




NYOTA 10 WALIOFUNGA HAT-TRICK MECHI YAO YA KWANZA UEFA UK. 12




# REKODI 5 ZA GUINNESS ALIZOWEKA RONALDO

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo ni mmoja wa wachezaji wakubwa wa mpira wa miguu waliowahi kucheza mchezo huo, ambaye ameweka urithi wake katika mchezo huu.

Nyota huyo wa Ureno amekuwa na tabia ya kuvunja rekodi mara kwa mara, na bado anaendelea kufanya hivyo.

Kwenye makala haya, tunaangalia rekodi tano kubwa za Guinness zinazoshikiliwa na Ronaldo, zifahamu sasa...

**#5. Mchezaji mkongwe kufunga hat-trick Kombe la Dunia**

Cristiano Ronaldo amekuwa hirizi na nyota wa Ureno kwa muda sasa, na mshambuliaji huyo alionyesha ubora wake tena kwenye Kombe la Dunia la mwaka 2018.

Ronaldo alifunga hat-trick dhidi ya Hispania akiwa na umri wa miaka 33, na kuhakikisha Ureno inatoka sare ya mabao 3-3 katika mchezo wa hatua ya makundi kwenye mashindano hayo. Hat-trick hii ni pamoja na 'free-kick' pia, na mshambuliaji huyo alisababisha shida kubwa kwa safu ya ulinzi ya Hispania.

Hata hivyo, Ronaldo hajapunguza kasi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alikuwa mfungaji bora wa Euro 2020 pamoja na Patrik Schick wa Jamhuri ya Czech, na hat-trick nyingine kwenye Kombe la Dunia la 2022 inaweza kutokea.

**#4. Kufunga michezo 11 mfululizo Uefa**

Ronaldo ni mmoja wa wachezaji waliopambwa sana katika historia ya mchezo huo, akiwa amekusanya mataji na tuzo binafsi kwa kiwango cha kushangaza.

Mchezaji huyo wa zamani wa Juventus ndiye mchezaji pekee kwenye mchezo huo aliyefunga katika mechi 11 mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ronaldo alipata mafanikio haya wakati akiwa na Real Madrid, na 'Los Blancos' hao bila shaka ndio ilikuwa timu bora wakati huo.

Ronaldo aliisaidia Real Madrid kushinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mara nyingi ikionekana kuwa ndiye anayesababisha tofauti.

**#3. Aliyetazamwa zaidi Wikipedia**

Ronaldo ni mmoja wa wanamichezo maarufu zaidi duniani na umaarufu wake unaenea zaidi ya ulimwengu wa mpira wa miguu. Uwepo wa mitandao ya kijamii ya Ronaldo umeandikwa vizuri.

Ni mmoja wa wanamichezo wanaofuatiliwa zaidi duniani na mikataba yake ya udhamini kwenye mitandao ya kijamii imekuwa ikifunikwa vizuri kwa miaka.

Ukurasa wa Wikipedia wa Ronaldo si tofauti. Ukurasa wa Wikipedia wa mshambuliaji huyo wa Manchester United ndio unaotazamwa zaidi kwa mwanamichezo wa kiume duniani na rekodi hii haishangazi.

**#2. Mabao mengi Ulaya**

Msimu wake akiwa Real Madrid, Ronaldo alikuwa wa kuvutia sana, na mshambuliaji huyo alikuwa akivunja rekodi wakati wote akiwa na klabu hiyo.

Ronaldo, ambaye ni mfungaji bora wa muda wote wa Real Madrid, aliweka rekodi nyingine wakati wa msimu wa 2013-14. Mchezaji huyo wa zamani wa Sporting CP alifunga mabao 17 katika mechi 11 tu za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huo, na hivyo kuwa mchezaji aliye na mabao mengi kwenye mashindano hayo ya Ulaya kwa msimu mmoja.

**#1. Mabao mengi kimataifa**


Mabao mawili ya Ronaldo dhidi ya Jamhuri ya Ireland siku chache zilizopita yalimfanya kuwa mfungaji bora wa muda wote wa kimataifa katika mpira wa miguu kwa wanaume.

Alivunja rekodi ya Ali Daei ya kufunga mabao mengi kwenye timu ya taifa na sasa ana mabao 111 katika mechi 180 kwa timu ya Ureno, rekodi ambayo inaonekana haiwezekani kuvunjwa wakati wowote hivi karibuni.

Uimara na maisha marefu ya Ronaldo mara nyingi yamethaminiwa, na mtu wa miaka 36 anajitunza vizuri. Mshambuliaji huyo anaonekana kuongeza malengo zaidi kwa idadi yake ya kimataifa, bila kuonyesha dalili za kupungua.

## ISIKUPITE

TANGU Ngao ya Jamii ianzishwe nchini mwaka 2001, Simba imeibeba mara tisa; 2002, 2003, 2005, 2011, 2012, 2017, 2018, 2019 na 2020. Yanga inafuatia kwa kuibeba mara sita; 2001, 2010, 2013, 2014, 2015 na 2021. Timu nyingine zilizoibeba ni Mtibwa Sugar 2009 na Azam FC 2016. Mwaka 2004 na 2006 hadi 2008 haikuchezwa.



Extra Time

# NYOTA 10 WALIOFUNGA HAT-TRICK MECHI YAO YA KWANZA UEFA



Haaland

**LONDON, England**

KATI ya matokeo maarufu, Manchester United ilikwama kwa Young Boys, na Barcelona ilipoteza nyumbani dhidi ya Bayern Munich. Kwingineko, mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Chelsea, Manchester City, Juventus na Real Madrid walifungua kampeni zao kwa kushinda.

Kulikuwa na maonyesho machache kibinafsi wakati wa wiki ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sebastien Haller na Christopher Nkunku walivutia na kufunga mabao matatu 'hat-tricks', kwenye mechi zao za kwanza.

Katika historia ya miaka kumi na tatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wachezaji 104 tofauti wamefunga hat-trick kwenye mashindano hayo. Lakini ni kumi tu kati yao wamefanya hivyo kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kwa hivyo bila kuchelewesha zaidi, wacha tuangalie wachezaji kumi waliofanya hivyo kwenye mechi zao za kwanza, twende sasa...

**#10. Sebastien Haller (Ajax) - 2021-22**

Sebastien Haller aliifanya mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kuwa tukio la kukumbukwa, wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alipofunga mabao manne katika ushindi wa 5-1 kwa Ajax kule Sporting Lisbon.

Mshambuliaji huyo wa Ivory Coast alijiunga na straika maarufu wa Uholanzi, Marco van Basten kama mchezaji pekee aliyefunga mara nne katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ni wachezaji wawili tu katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wamefunga mabao manne kwenye mechi yao ya kwanza.

#9. Mislav Orsic (Dinamo Zagreb) - 2019-20

Mislav Orsic alifunga mara tatu dhidi ya wakuja kwenye mashindano hayo Atalanta katika ushindi wa mabao 4-0 nyumbani kwa Dinamo Zagreb kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ya msimu wa 2019-20.

Kiungo huyo alifunga mara mbili katika kipindi cha kwanza kabla ya kumalizia hat-trick yake katikati ya kipindi cha pili.

Mabao ya Orsic yaliifanya Croatia kuwa nchi ya 17 tofauti kufunga kwenye mashindano hayo na Dinamo Zagreb kuwa klabu ya 47 tofauti kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Orsic ni mwenye umri wa miaka 28, pia ni mchezaji wa kwanza wa Dinamo Zagreb kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Orsic hivi karibuni alifunga hat-trick nyingine kwenye Ligi ya Europa, akifunga mara tatu dhidi ya Tottenham Hotspur katika Ligi ya Europa msimu uliopita. Hiyo ilimfanya mchezaji huyo kuwa wa pili kufunga hat-trick ya Europa dhidi ya Spurs.

**#8. Erling Haaland (Salzburg) - 2019-20**

Erling Haaland aliichukua Ligi ya Mabingwa Ulaya kama samaki kwenye maji wakati kijana huyo wa miaka 19, alipofunga mara tatu katika ushindi wa mabao 6-2 wa Salzburg dhidi ya Genk.

Hiyo ilimfanya Haaland (akiwa na miaka 19 na siku 58) kuwa mchezaji wa tatu mwenye umri mdogo zaidi kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa. Raul tu wa Real Madrid (akiwa na miaka 18 na siku 113) na Wayne Rooney (miaka 18 na siku 340) walikuwa wadogo kuliko raia huyo wa Norway walipofunga mara tatu kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Haaland ni mchezaji wa tatu wa Norway kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Na pia aliifanya Salzburg kuwa klabu ya kwanza kutoka Austria kufunga hat-trick kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ssa akiwa kule Borussia Dortmund, Haaland tayari ana mabao 20 kwenye mashindano hayo. Haaland alifunga mabao kumi katika kila kampeni zake mbili za mwisho kwenye mashindano hayo. Alifungua akaunti yake ya msimu kwa kufunga bao katika ushindi wa mabao 3-2 wa Dortmund dhidi ya Besiktas.

**#7. Yacine Brahimi (Porto) - 2014-15**

Yacine Brahimi alifunga hat-trick ya 91 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati alipofunga mabao matatu kwa Porto dhidi ya BATE Borisov msimu wa 2014-15. Hiyo ilimfanya Brahimi kuwa mchezaji wa kwanza wa Algeria na Porto kuwa klabu ya 42 tofauti kufunga hat-trick kwenye mashindano hayo.

Alifunga mara mbili ndani ya dakika 32 za ufunguzi. Brahimi kisha alikamilisha hat-trick yake dakika 12 katika kipindi cha pili wakati Porto ikishinda mabao 6-0.

Katika harakati hizo, raia huyo wa Algeria mwenye umri wa miaka 24 alikuwa mchezaji mchanga zaidi wa Afrika baada ya Yakubu wa Nigeria (miaka 19) kufunga mabao matatu kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#6. Grafite (Wolfsburg) - 2009-10**

Grafite alikuwa mchezaji wa nane wa Brazil kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati alipofunga mara tatu kwa VfL Wolfsburg dhidi ya CSKA Moscow kwenye mchezo wa msimu wa 2009-10.

Ilikuwa hat-trick ya 60 kwenye mashindano hayo, kwani Wolfsburg ikawa ni timu tofauti ya 39 kusajili hat-trick kwenye mashindano hayo. Mshambuliaji huyo wa Brazil alifunga mabao yote matatu wakati mabingwa hao wa Bundesliga walipofungua kampeni yao na ushindi wa 3-1 dhidi ya CSKA Moscow.

Grafite ndiye mchezaji mkongwe wa Brazil kufunga mara tatu katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#5. Vincenzo Iaquinta (Udinese) - 2005-06**

Vincenzo Laquinta alifunga hat-trick ya 48 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika ushindi wa mabao 3-0 wa Udinese dhidi ya Panathinaikos kwenye mchezo wa makundi wa msimu wa 2005-06.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2006, ni mchezaji wa tano na wa hivi karibuni wa Italia kufunga mara tatu kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mabao matatu ya Laquinta yaliifanya Udinese kuwa klabu ya 35 tofauti kupata hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Amefunga mabao nane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika michezo 12, na manne kati yao akiichezea Juventus.

**#4. Wayne Rooney (Manchester United) - 2003-04**

Wayne Rooney ndiye Muingereza wa kwanza kufunga hat-trick kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifanya hivyo wakati alipofunga mara tatu katika ushindi wa mabao 6-2 wa Manchester United dhidi ya Fenerbahce msimu wa 2004-05.

Rooney akiwa na umri wa miaka 18 wakati huo, pia alitoa msaada mkubwa kwa United ikipata ushindi mkubwa pale Old Trafford. Hiyo ilikuwa hat-trick pekee ya kwenye mashindano hayo.

Rooney 85 ya Ligi ya alifunga mabao 30 katika michezo Mabingwa Ulaya, yote kwa Man United. Bao lake la mwisho kwenye mashindano hayo lilikuja dhidi ya CSKA mwaka 2015.

**#3. Yakubu (Maccabi Haifa) - 2002-03**

Yakubu alifunga hat-trick kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2002-03. Mshambuliaji huyo wa Nigeria alifunga mara tatu kwa Maccabi Haifa katika ushindi wao wa mabao 3-0 nyumbani dhidi ya Olympiacos katika mchezo wa makundi.

Ilikuwa hat-trick ya 33 kwenye mashindano na ya kwanza kufanywa na mchezaji wa Kiafrika. Maccabi Haifa alikuwa klabu ya kwanza kutoka Israeli kupata hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa bahati mbaya, Yakubu alifunga mara mbili tu kwenye mechi zote za mashindano kwa Maccabi Haifa.

**#2. Faustino Asprilla (Newcastle United) - 1997-98**

Faustino Asprilla alifunga hat-trick ya 12 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifunga mara tatu katika ushindi wa mabao 3-2 nyumbani kwa Newcastle United dhidi ya Barcelona katika mchezo wa makundi msimu wa 1997-98.

Mabao hayo yalimfanya Asprilla kuwa mchezaji wa kwanza kutoka Amerika Kusini tangu Romario kufunga mara tatu katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Asprilla na Andriy Shevchenko (pia msimu wa 1997-98) walikuwa wachezaji pekee kufunga hat-trick ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona kabla ya Kylian Mbappe kujiunga nao hivi karibuni.

Mbappe ndiye mchezaji wa tatu tu kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona, baada ya Faustino Asprilla kwa Newcastle na Andriy Shevchenko kwa Dynamo Kyiv (wote mwaka 1997).

**#1. Marco van Basten (AC Milan) - 1992-93**


Gwiji wa AC Milan Marco van Basten ndiye mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifunga hat-trick ya tatu kabisa kwenye Ligi ya Mabingwa wakati alipofunga mabao yote manne katika ushindi wa 4-0 wa Milan dhidi ya IFK Goteborg katika mchezo wa makundi msimu wa 1992-93.

Kwa karibu miongo mitatu, mshambuliaji huyo maarufu wa Uholanzi, alibaki kuwa mchezaji pekee kufunga mara nne katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ilikuwa hadi Sebastien Haller alipojiunga naye kwa kufunga mara nne dhidi ya Sporting Lisbon siku ya kwanza ya mechi ya msimu wa 2021-22.

Van Basten alijiunga na mwenzake Juul Ellerman kama Mholanzi pekee aliyefunga mabao matatu kwenye mchezo wa michuano hiyo. Ellerman ndiye mfungaji wa hat-trick ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## Nukuu

"Hakuna mtu aliyefadhaika na kuumia moyoni kuliko mimi kwa kukosa penalti na kufungwa. Leo, nilishindwa. Lakini ninapiga hatua mbele na kukabiliwa na changamoto hiyo na azma na jukumu kama hilo na kwenye matukio mengine, mpira uliishia kwenye wavu," **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes baada ya kukosa penalti wakati wakilala kwa bao 1-0 dhidi ya Aston Villa juzi.**



"N'Golo ni N'Golo, ni wa kipekee, wa aina yake na kuwa naye uwanjani hufanya tofauti kubwa kwa kila kitu na una kila kitu mtu anatafuta. Kuwa na Kante kwenye kikosi ni sehemu ya kufurahisha, kwa sababu anaweza kufanya chochote wakati wowote, kwa hakika ni mmoja wa wachezaji muhimu sana kwenye kikosi changu," **Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel**



"KAMA nitatakiwa kuchagua Ronaldo [Cristiano] ama Lukaku [Romelu] nani nimchezesha kama mshambuliaji wa kati, kutakuwa hakuna mjadala. Itakuwa ni Lukaku mara zote**," Nyota wa zamani wa Manchester United, Garth Crooks**



# YANGA WABABE NGAO YA JAMII DHIDI YA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI aliyesajiliwa msimu huu kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fiston Mayele, ndiye aliyewalaza mapema Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, alipoifungia Yanga bao pekee kwenye mechi ya watani wa jadi, ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 11, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Farid Mussa aliyewatoka walinzi kadhaa wa Simba na kummegea pande mfungaji, ambaye hakutuliza huku Aishi Manula akiruka, lakini alipishana na mpira huo ukijaa wavuni.

Simba ikacheza kwa dakika 79 bila kupata bao lolote na kuifanya Yanga kutwaa Ngao ya Jamii kwa mara ya kwanza baada ya miaka sita. Mara ya mwisho Yanga kutwaa Ngao ya Jamii ilikuwa mwaka 2015 ilipoifunga Azam FC kwa mikwaju ya penalti 8-7.

Mayowe, nderemo na furaha za wanachama na mashabiki wa Yanga zilirindima uwanjani baada ya nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto alipokabidhiwa ngao hiyo, ikiwa sasa ni ishara ya kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22.

Katika makala haya tunatazama rekodi na takwimu za Yanga kwenye mechi za Ngao ya Jamii dhidi ya Simba iliyobeba taji hilo mara tisa. Baada ya ushindi wa jana, Yanga sasa imebeba mara sita.

Yanga ilianza kutwaa Ngao ya Jamii mwaka 2001, baada ya hapo ikaja 2010, 2013, 2014, 2015 na sasa 2021, huku watani zao wakiwa wametwaa 2002, 2003, 2005, 2011, 2012, 2017, 2018, 2019 na 2020. Hii inakuwa ni mechi ya tano kwa Simba na Yanga kukutana kwenye Ngao ya Jamii, Yanga ikishinda mara tatu na Simba mara mbili.

**Hapa tunatazama matokeo matano ya mechi hizo za watani wa jadi, twende sasa...**



Straika wa Yanga, Fiston Mayele, akishangilia baada ya kuiua Simba Uwanja wa Mkapa juzi kwenye mechi ya Ngao ya Jamii. Chini ni Shomari Kapombe na pembeni ni Paschal Wawa na Joash Onyango. **MPIGAPICHA WETU**

**Yanga 2-1 Simba (2001)**

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Simba na Yanga kukutana kwenye Ngao ya Jamii na Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-1. Ilichezwa Februari 17, 2001, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Simba ilianza kupata bao likifungwa na Steven Mapunnda 'Garincha' dakika ya 43, Yanga ikisawazisha kupitia kwa Edibilly Lunyamila dakika ya 47, Ally Yusuph 'Tigana' akifunga bao la ushindi dakika ya 80.

**Yanga 3-1 (penalti) Simba (2010)**

Timu hizo zilikutana tena Agosti 18, 2010 Uwanja wa Taifa (sasa Benjamin Mkapa). Ni mechi iliyoshuhudia kwa mara nyingine tena Yanga ikitwaa Ngao ya Jamii mbele ya Simba, baada ya kushinda mabao 3-1 kwa mikwaju ya penalti kutokana na dakika 90 kumalizi kwa suluhu.

Penalti za Yanga ziliwekwa wavuni na marehemu Geofrey Bonny, Stephano Mwasika na Isack Boakye, huku pekee ya Simba ikifungwa na Mohamed Banka.

Ernest Boakye alikosa penalti kwa upande wa Yanga, Emmanuel Okwi, Uhuru Selemani na Juma Nyosso wakikosa kwa upande wa Simba.

**Simba 2-0 Yanga (2011)**

Simba ilitwaa Ngao ya Jamii mbele ya Yanga kwa mara ya kwanza 2011, mechi ikichezwa Agosti 17, Uwanja wa Taifa Dar es saalaam (Mkapa). Simba ikiondoka uwanjani na ushindi wa mabao 2-0. Yalikuwa ni mabao ya Haruna Moshi 'Boban' na Mzambia Felix Sunzu.

**Simba 5-4 (penalti) Yanga (2017)**

Zilikutana tena 2017 kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi msimu wa 2017/18, Simba ikishinda kwa mabao 5-4 kwa mikwaju ya penalti.

Penalti za Simba zilikandamizwa na Method Mwanjali, Haruna Niyonzima, Emmanuel Okwi, Shiza Kichuya na Mohamed Ibrahim huku za Yanga zikifungwa na Papy Tshishimbi, Thaban Kamusoko, Ibrahim Ajibu na Donald Ngoma.

**Yanga 1-0 Simba (2021)**

Miaka minne baadaye, hatimaye timu hizo zimekutana tena Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa na Yanga kushinda bao 1-0, ikitwaa Ngao ya Jamii mara nyingi mbele ya mahasimu wao wa jadi, Simba.

**JE, WAJUA?**



NI makocha wawili tu kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), waliowahi kutwaa kombe hilo mara tatu; Charles Gyamfi akiwa na Ghana mwaka 1982, 1965 na 1963. Kocha mwingine ni Hassan Shehata akiwa na Misri mwaka 2006, 2008 na 2010. Je, nani atawafuata?





# Wakurugenzi waagizwa kutumia EFD

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAKURUGENZI wa halmashauri nchini, wametakiwa kutumia mashine za kielektroniki (EFD) kukusanya mapato badala ya kutumia risiti za kuandikwa kwa mkono, kwa kuwa zinachangia upotevu wa fedha.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliyasema hayo alipokuwa akifunga mafunzo elekezi kwa wakurugenzi hao, jijini hapa.

Alisema wanapaswa kuhakikisha hawakusanyi mapato kwa risiti zinazoandikwa kwa kuwa zinatoa mwanya wa kupoteza mapato.

Silinde alisema bado kuna maeneo fedha za serikali zinapotea na kuingia katika mifuko ya wajanja kwa kutumia risiti za mikono.

"Nataka mhakikishe mnatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na mkaongeze kasi ya ukusanyaji mapato kwa kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji usioumiza watoaji wa mapato," alisema.

Alisisitiza matumizi sahihi ya fedha bila kuvunja sheria na zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kulingana na thamani ya fedha zilizotumika ikilinganishwa na huduma iliyotolewa.

"Kumbukeni mwisho wa kila mwaka serikali inafanya ukaguzi, hivyo ni vyema kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato, lakini kuongeza nidhamu katika matumizi," alisema. Aliwataka kusimamia nidhamu na kuhakikisha wanatenda kwa watumishi wanaowaongoza.

"Zingatieni mipaka ya madaraka na kazi na kuwa hatua watakazozichukua katika utendaji wa majukumu yao inapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi katika utumishi wa umma na serikali kwa ujumla," alisema.

Naibu Waziri huyo alihimiza wakurugenzi hao kwenda kutatua kero za wananchi na kuwataka wahakikishe wanapatikana kirahisi ofisini na kuondoa urasimu.

"Uteuzi wenu kwenye nyadhifa, madaraka na mamlaka mliokabidhiwa yanalenga katika kutatua kero na matatizo ya wananchi hivyo mnapaswa kukerwa sana na matatizo ya wananchi, hususani wale wa vijijini ambao wengi wao ni maskini," alisema.

Aliwataka kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vituo vya afya na vituo vya majisafi na salama.

Awali, Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Nuru Namoroma, alisema katika kikao kazi hicho mada 21 zimetolewa ambazo zimelenga kuwawezesha kujifunza mambo mengi ambayo ni msingi wa utekelezaji wa majukumu yao.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (kushoto), pamoja na Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri nchini, Dk. Aggrey Mlimuka (katikati), wakikabidhi hati za makubaliano kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwandani, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Boniphace Nkakatisi, baada ya kutia saini mkataba wa hiari wa Hali Bora baina ya Menejimenti ya kampuni za ORYX Energies na TUICO jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chamuriho ataja mafanikio ya Mpango wa Maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi, imeendelea kutekeleza kwa mafanikio Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) kwa kukamilisha miradi mbalimbali, ikiwamo ujenzi wa madaraja makubwa tisa.

Aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Leonard Chamuriho, aliyasema mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati wa kumkabidhi ofisi na Waziri mpya, Prof. Makame Mbarawa, aliyeteuliwa hivi karibuni.

Alitaja madaraja hayo kuwa ni daraja la Magufuli (Kilombero), Nyerere (Kigamboni -Dar es Salaam), Magara (Manyara), Kavuu (Katavi), Mlalakuwa (Dar es Salaam), Momba (Rukwa), Lukuledi (Lindi), Mara (Mara) na Sibiti mkoani Singida.

Aidha, Mhandisi Chamuriho alisema daraja jipya la Selander, daraja la Msingi (Singida), daraja jipya la Wami, Kitengule, Ruhuhu na Kigongo - Busisi, ujenzi wake unaendelea na upo katika hatua nzuri.

Akizungumzia kuhusu usafiri wa anga, alisema jumla ya ndege 11 zimenunuliwa na tayari mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine mpya tano umeshafanyika.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alimwomba Chamuriho kuendelea kushirikiana na wizara hiyo, ili kuwatumikia vyema Watanzania.

"Mheshimiwa Chamuriho wewe ni kiongozi makini, mwenye utaalamu na ambaye umefanya mambo makubwa nchini kwa weledi katika kuhakikisha Watan zania wanapata miundombinu iliyo bora," alisema Prof. Makame.

# Sheria, kanuni sekta ya uvuvi kuboreshwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI inafanya mapitio ya sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya uvuvi ili kukuza na kuendeleza viumbe maji.

Moja ya njia za kukuza na kuendeleza viumbe hai ni pamoja na ufugaji samaki kwa kutumia vizimba.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alibainisha hayo jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kushiriki mkutano wa kimataifa wa kukuza na kuendeleza ukuzaji viumbe maji ulifanyika kwa njia ya mtandao.

Mashimba, alisema lengo la kupitia sheria pamoja na kanuni katika sekta hiyo ni kuhakikisha kuwa zinawezesha uvuvi wa kutumia vizimba pamoja na mabwawa.

"Sheria pamoja na kanuni zetu awali sekta hii ya uvuvi ilikuwa imemezwa na uvuvi wa majini tuu hivyo tunafanya mapitio ili kuwezesha uvuvi huu wa kutumia vizimba unakuwa na mchango katika kuongeza pato la taifa," alisema Mashimba.

Akizungumzia mkutano huo, alisema lengo lake ni kuwezesha nchi washiriki kukuza na kuendelea ukuzaji wa viumbe maji kwa kutumia uvuvi wa vizimba, mabwawa pamoja na njia nyingene zisikuwa za bahari au ziwa.

"Pia katika mkutano huu tunaangalia changamoto pamoja na fursa zilizopo, vipaumbele na namna ya kuendeleza uvuvi wa viumbe maji," alisema.

Alisema uvuvi huo una mchango mkubwa katika usalama wa chakula ambapo hivi sasa sekta hiyo inachangia pato la taifa kwa asilimia 1.7.

"Kwenye samaki tunapata protini kwa asilimia 21 na takwimu zinaonyesha kuwa kuna kipindi tulipanda hadi kufikia mtu mmoja kula kilo 14, kwa mwaka lakini mwaka 2020, tumeshuka hadi mtu mmoja kula kilo 8.5 kwa mwaka," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema Taifa linatakiwa kuwa na uvuvi endelevu unaochangia usalama wa chakula na kukabiliana na mabadiliko tabianchi.

"Tumekubaliana kuwa na ushirikiano wetu wa namna ya kupeana utaalamu wa kukabiliana na mabadiliko tabianchi ili kuwa na uvuvi endelevu utakaokuza pato letu lakini pia pato la dunia kupitia sekta hii," alisisitiza.

Vilevile, alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha inafanya utafiti wa maeneo kwa ajili ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba.

"Ili kuwasaidia watu wanaohitaji kufuga samaki kwa njia hii serikali inafanya utafiti wa mazingira kwa ajili ya ufugaji ili kuwaondolea gharama wananchi watakaohitaji kwa kuwa gharama zake ni kubwa," alisema.

Kadhalika, alisema mkakati mwingine ni kuhakikisha kuwa vituo vitano vya ukuzaji viumbe maji vinaboresha na kuzalisha vifaranga vya samaki kwa wingi na vyenye ubora.

"Lakini serikali inampango wa kuanzisha mashamba darasa kila wilaya kwa ajili ya kufundisha wakulima pamoja na wafugaji ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba na mabwawa," alisema.





Baadhi ya vijana wa mji wa Mbalizi mkoani Mbeya wakisafirisha mikungu ya ndizi kwa baiskeli kutoka kwenye mashamba yaliyoko Utengule kupeleka soko la Tarafani mkoani humo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ujenzi wa kiwanda kuchakata mboga na matunda waanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya mboga na matunda ili kuongeza thamani ya mazao hayo kabla ya kuyauza katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Lengo lingine la ujenzi huo limetajwa kuwa ni kupunguza upotevu wa mazao hayo baada ya kuvuna.

Ujenzi wa kiwanda hicho ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa kupitia programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani kwenye kahawa, chai, matunda na mboga ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT chini ya Ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Mkurugenzi wa Shirika la HELVETAS Tanzania, Daniel Kalimbiya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati kamati ya utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na shirika hilo pamoja na Shirika la RICOLTO ilipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa kiwanda hicho.

Kiwanda hicho kinajengwa katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani uliopo Kata ya Iyela jijini Mbeya, ambapo Kalimbiya alisema ujenzi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni moja mpaka kukamilika kwake na kwamba kitakuwa kiwanda kikubwa kuliko vyote katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema katika eneo hilo pia zitakuwapo taasisi mbalimbali za kuthibitisha ubora wa mazao hayo pamoja na maduka ya kisasa ya kuuzia bidhaa hizo ambayo yatakuwa na wajasiriamali zaidi ya 200 ambao watakuwa wanafanya shughuli zao hapo.

"Ujenzi huu utakamilika baada ya miezi minane, lakini kiwanda hiki kitakuwa kikubwa sana, kitawasaidia wakulima wa mazao ya bustani hasa mboga na matunda kupunguza upotevu wa mazao yao wakati wa mavuno," alisema Kalimbiya.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji wa miradi hiyo, Juma Homera ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, aliyaagiza mashirika hayo yasiyokuwa ya kiserikali kuhakikisha yanakamilisha ujenzi wa kiwanda hicho haraka na kwa viwango vinavyotakiwa.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kujipanga kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa maelezo kuwa soko litakuwa la uhakika kutokana na uwepo wa kiwanda hicho na kwamba serikali inaendelea kuboresha miundombinu kwa ajili ya usafirishaji.

Homera Programu ya AGRI-CONNECT inaungwa mkono na serikali kutokana na miradi ambayo inatekelezwa kuwa na umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya taifa ikiwemo uboreshaji wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na wakala wa barabara za vijijini (TARURA).

"Nawaomba wananchi waanze kujiandaa kuzalisha mazao haya kwa wingi ili kiwanda hiki kije kiwe na faida kwao, kwa sasa Serikali inaboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), lakini yatajengwa majengo ya maridi (cold rooms) kwa ajili ya kuhidadhia matunda na mboga kabla ya kusafirishwa," alisema Homera.

Vilevile, alisema hivi karibuni mabalozi wanane wa Umoja wa Ulaya (EU) walifanya ziara katika mkoa huo kwa ajili ya kutembelea miradi yote ambayo inafadhiliwa na umoja huo pamoja na nchi wanachama wake na kwamba waliridhika na utekelezaji huo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka watekelezaji wa miradi hiyo kuwa waaminifu ili wananchi wanufaike pamoja na kuepuka wafadhili kusitisha ufadhili huo.

Aliwataka kutekeleza miradi hiyo kulingana na matakwa ya wafadhili na kwamba wahakikishe wanatoa taarifa ya utekelezaji kwa wakuu wa Wilaya na wakurugenzi wa Halmashauri ambazo miradi hiyo inatekelezwa kwa ajili ya ufuatiliaji.

Shirika la HELVETAS linatekeleza miradi hiyo kupitia mradi wake wa KIBOWAVI huku RICOLTO wakitekeleza kupitia mradi wa BICHOBS.

## Chanjo yasitisha likizo za madaktari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesitisha likizo zote za waganga wakuu wa halmashauri zote mkoani humo ili wasimamie chanjo dhidi ya virusi vya corona.

Hopmera pia amewaagiza waganga ambao wako likizo kurejea kazini mara moja.

Aidha, Homera amewazuia wakuu hao kutosafiri nje ya wilaya zao mpaka zoezi hilo litakapokamilika, na kwamba wanatakiwa wahakikishe wanahamasisha wananchi kujitokeza kuchanja ili dozi zote zilizotolewa kwa ajili ya mkoa huo ziishe.

Akizungumza kwenye mafunzo ya Kamati ya Afya ya Msingi ya Mkoa huo kuhusu chanjo dhidi ya corona, Homera alisema utoaji chanjo limeonekana kusuasua katika mkoa huo, kutokana na elimu ndogo kwa wananchi pamoja na uwajibikaji mdogo wa waganga wakuu.

Aliwataka kila halmashauri kuandaa gari maalum la matangazo ambalo litakuwa linatumika kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchanja na kwamba kwenye maeneo yote ya mikusanyiko lazima chanjo zipelekwe na wananchi wahamasishwe kuchanja.

"Chanjo zipelekwe sehemu yoyote ya mkusanyiko, hata kwenye makanisa na misikiti watu wakahamasishwe kuchanja, kila halmashauri angalau ichanje watu 100 kwa siku," alisema Homera.

Alitahadharisha kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wote watakaotoa taarifa za upotoshaji kuhusu chanjo hiyo ili kuhakikisha zoezi hilo la uchanjaji linafanyika kwa usahihi.

Alisema chanjo ya corona inamwezesha mtu kutopata maambukizi kwa urahisi, na kwamba hata akipata hawezi kudhurika kama yule ambaye hajachanjwa.

# TCB yakopesha wanawake bil. 128/- kukuza uchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) imewakopesha wanawake zaidi ya Sh. bilioni 128 kwa nyakati tofauti kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za ujasiriamali pamoja na biashara kubwa ili kukuza uchumi wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kufunga kongamano maalum la wanawake wajasiriamali wa Mkoa wa Mbeya lililokuwa limeandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya kuwafundisha fursa mbalimbali za ujasiriamali wanawake hao zilizopo mkoani humo.

Alisema mikopo hiyo inajumuisha mikopo ya wanawake wajasiriamali wadogo wadogo, vikundi pamoja na wafanyabiashara wakubwa wanaowekeza kwenye biashara zikiwamo za kimataifa pamoja na viwanda.

Alisema wafanyabiashara wakubwa wamekopeshwa zaidi ya Sh. bilioni 100 huku wajasiriamali wadogo wakiwa wamekopeshwa zaidi ya Sh. bilioni 28, na kwamba kundi hilo la wanawake limekuwa likifanya vizuri kwenye urejeshaji.

Alisema benki hiyo imekuwa na wateja wengi wanawake kutokana na kundi hilo kuaminika kwa kukopa na kurejesha fedha kwa wakati na kwamba kundi hilo ni miongoni mwa makundi ambayo benki zao ziliunganishwa na benki hiyo hivi karibuni.

"Kwenye kongamano hili mbali na kuwaelekeza wanawake hawa fursa mbalimbali za uwekezaji, lakini wamefundishwa mambo mbalimbali ikiwamo mbinu za uendeshaji wa biashara zao pamoja na matumizi sahihi ya fedha ili kukuza biashara zao," alisema Moshingi.

Alisema kongamano hilo limekuwa la pili kufanyika mkoani Mbeya baada ya lile la awali kufanyika jijini Dodoma na kwamba wataendelea kufanya hata katika mikoa mingine ya Tanzania kwa maelezo kuwa benki hiyo ina matawi katika mikoa yote.

Alisema TCB ina zaidi ya matawi 80 katika nchi nzima na kwamba baadhi ya matawi ni makubwa na mengine ni madogo kulingana na eneo husika.

Akifunga kongamano hilo Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliwataka wanawake hao kufanya kazi kwa bidii ili kujiongezea kipato na kwamba hawatakiwi kukata tama pale biashara zao zinapoteteleka bali wanatakiwa kujifunza.

Aliwataka kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza zikiwamo za mafunzo ili wakuze biashara zao na kwamba hawatakiwi kuishia kuwa wajasiriamali bali wafikie hatua wawe wafanyabiashara wakubwa.

"Mimi mwenyewe pamoja na nafasi niliyonayo serikalini, lakini bado ni mjasiriamali, mimi ni mama ntilie, kwahiyo nawatia moyo wajasiriamali wenzangu tusikate tamaa, hii benki imekuja kutufungua macho ili tuzione fursa ambazo tulikuwa hatuzioni," alisema Mahundi.

Aliwataka wanawake hao kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha, ili wafanikiwe zaidi kwa maelezo kuwa hawatakiwi kujikita zaidi kwenye ununuzi wa nguo na vitu vingine vya anasa.

Kongamano hilo lilifunguliwa na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, ambaye alizishauri taasisi za fedha kufanya tathmini ya biashara za wananchi kabla ya kuwakopesha mikopo wanayohitaji ili mikopo hiyo iwasaidie badala ya kuwadidimiza.



## HABARI ZANZIBAR

# RPC mpya aahidi kuendeleza amani Mjini Magharibi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMANDA wa Mkoa wa Kagera Kamishna Msaidizi wa Polisi, Awadh Juma Haji, amewaomba wanahabari kumpa ushirikiano kamanda mpya wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ambao amemaliza kuuongoza, ili kuhakikisha wanaendelea kupambana na matendo yote ya kihalifu.

Aliyasema hayo jana wakati akimtambulisha Kamanda mpya wa mkoa huo, Omar Said Nassir, kwa waandishi wa habari, mjini hapa.

Alisema wanahabari ni wadau muhimu katika mkoa huo na walikuwa na ushirikiano makubwa na Jeshi la Polisi katika kutoa taarifa mbalimbali za kiuhalifu na matukio mengine ambayo yalikuwa yakijitokeza.

Kamanda Awadhi, aliwahakikishia wanahabari kuwa Kamanda Omar anautendaji mzuri na yupo tayari kushirikiana wakati wote wanapomuhitaji ili na yeye aweze kuendeleza jukumu hilo la kupambana na uhalifu na wahalifu katika mkoa huo.

"Kamanda huyu ana uwezo mkubwa na naamini mtashirikiana naye kwa karibu na atadhibiti maeneo ya uhalifu na atakwenda kwa kasi kubwa zaidi ili mkoa ubaki salama," alisema.

Aliwashukuru wanahabari kwa ushirikiano mkubwa waliompa katika kipindi chote alichofanya kazi katika mkoa huo kwa kushirikiana pamoja ili mkoa huo uwe shwari anapomkabidhi kijiti hicho.

"Kwa kweli nina deni kubwa kwenu wanahabari mlikuwa mkinipa ushirikiano mkubwa naamini na huyu mwenzangu mtampa ushirikiano na namkabidhi mwenzangu kijiti hiki ili na yeye aweze kuendeleza mapambano haya ya uhalifu na kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanaendelea kuishi kwa hali ya amani na utulivu mkubwa," alisema.

Kamanda Awadh, alibainisha kwamba mapambano hayo hayakuwa yake pekee bali alikuwa akishirikiana na askari wenzake na watumishi wengine ambao alishirikiana nao kuhakikisha mkoa unakuwa salama wakati wote.

Aliwashukuru wananchi wote wa mkoa huo kwa namna ya kipekee kulisaidia jeshi katika mapambano dhidi ya uhalifu na kusaidia katika hali zote kuhakikisha vitendo vya uhalifu vinaondoka katika mkoa huo.

Alipongeza vikosi vingine vya ulinzi na usalama, wadau mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara na viongozi wa serikali katika ushirikiano waliompatia wakati akihudumu nafasi hiyo mkoani humo.

Naye Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Omar Said Nassir, alimpongeza Kamanda Awadh kwa msaada aliompa ambao utamwezesha kuanza kazi zake vizuri.

Aliahidi kushirikiana na vyombo vya habari wakati wote na kusema ana deni kubwa kwa watu wa mkoa huo ili kuhakikisha unakuwa na amani na utulivu wakati wote.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Awadh Haji Juma (kushoto), akiagana na kamanda mpya wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Omar Nassir, ofisini kwake Mwembe Madema Mjini Zanzibar, baada ya kumaliza kufanya kazi mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kuhamishiwa Kagera. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mjumbe ACT-Wazalendo ataka SUK iungwe mkono

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa Wazanzibari wote kuendelea kuunga mkono maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwa kufanya hivyo ndio kupigania maslahi ya Zanzibar.

Othman, ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana kwenye ziara maalum ya kutembelea Baraza la Chama hicho katika Jimbo la Malindi Mjini Unguja. Alisema kuunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kila Mzanzibari ni jambo muhimu ambalo litaacha urithi mzuri wa mshikamano na amani ya nchi kwa kizazi cha sasa na kijacho na kuifanya nchi kuwa imara zaidi.

Alisema uamuzi wa Chama cha ACT kushiriki katika serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa umetokana na mashauriano ya wanachama na viongozi na kukubalika kwake kumetokana na kujali maslahi na maendeleo ya nchi zaidi.

Aliwataka wanachama wa chama hicho pamoja na wananchi kwa jumla, kuendelea kudumisha amani na mshikamano wa nchi, huku viongozi wakiendelea kufanya juhudi za kujenga misingi bora na imara ya kuendeleza serikali hiyo.

Alisema mapendekezo ya msingi na mashauriano ya kuimarisha zaidi serikali hiyo yamefanywa na kujadiliwa katika ngazi ya chama hicho, ambayo yanatarajiwa iwapo yatakubalika yatasaidia kujenga misingi imara na bora zaidi ya kuendeleza serikali hiyo na kuweka mustakabali mwema wa Zanzibar.

Othman alitembelea baraza za chama hicho katika maeneo ya Mji Mkongwe ikiwamo ya Jaws Corner ya soko Muhogo, eneo la Makaburi ya wanawazuoni lililopo Ukutani, Msaji eneo la Kokoni, Darajani, Mtendeni na Common Wealthy iliyopo Michenzani mjini Unguja.

Aidha, katika baraza alizotembelea ameombwa na wanachama hao kuwa mlezi na amekubali kuendeleza jitihada za pamoja za kujenga ummoja na maelewano ya Zanzibar.

# ZAHRI yatakiwa kuendeleza utafiti dawa asili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), imetakiwa kuendeleza utafiti wa dawa za asili ili zitumike kwa usahihi katika kutibu maradhi yasiyoambukiza.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi wa uongezaji wa thamani tiba za mimea ya asili katika kutibu maradhi yasiyoambukiza ofisini kwake Mnazi Moja, Mkurugenzi Tiba kutoka Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Amour Suleiman Mohamed, alisema utafiti uliofanywa utawasaidia wanajamii kutibu maradhi ya kuambukiza kwa usahihi na kuepuka kubahatisha.

Alisema kuwa, idadi kubwa ya wanajamii hutumia dawa za asili bila kuwa na elimu na kipimo sahihi jambo ambalo husababisha madhara makubwa kwa afya zao.

Alisema ili kuiepusha jamii na madhara hayo, ipo haja ya kutoa elimu ya viwango na matumizi sahihi ya dawa hizo ili kuleta matokeo chanya ya dawa zinazotumiwa.

"Jamii hutumia dawa asili za mimea bila kiwango, kupitia utafiti hizi zitasaidia kugundua maradhi na kutumia tiba kwa kiwango kinachopatikana ili kuwasaidia wazee wetu majumbani kuweza kutumia dawa kwa usahihi kulingana na majibu sahihi yanayotolewa na tafiti ili kuleta tija," alisema Dk. Amour.

Alisema kuwa, dunia ilipokumbwa na janga la Uviko-19 tiba asili zilisaidia kupambana na janga hilo na kwamba ni vyema kuongeza jitihada katika kuzipa thamani dawa hizo za mimea na kuzitumia kama zinavyotumika katika nchini nyingine.

Kwa upande wake, Mwenyekiti Baraza la Tiba Asili, Profesa Hamis Malebo, alisema jamii inapaswa kupewa elimu kuhusu kuhifadhi na kutunza rasilimali ya mimea dawa, kwa kuwa inamchango mkubwa katika kuimarisha sekta ya afya nchini.

Aliipongeza Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar, kwa kuchukua fursa hiyo muhimu ya kuanzisha mradi huo utakaosaidia kuonyesha thamani ya dawa asili zinazotokana na mimea.

# Serikali yaombwa elimu kwa wachimbaji madini

**Na Yasmine Protace**

WASHIRIKI wa semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), wameomba serikali iendelee kutoa elimu kwa wachimba madini ili kunufaika nayo.

Hayo yalisemwa na mmoja wa washiriki wa semina hizo, Hawa Juma, alipokuwa akichangia mada kuhusu taarifa za mapato katika sekta ya madini.

Alisema kuna madini ya aina mbalimbali na yanaliletea taifa mapato, lakini kinachotakiwa ni kuwapo na utaratibu wa kutoa taarifa za mapato ukiwamo uuzwaji wake.

Amina Juma alisema kinachotakiwa ni kutolewa kwa elimu kwa wachimbaji na kwamba elimu bora inapotolewa wachimbaji wananufaika na masoko.

"Elimu bora inapotolewa kwa wachimbaji itasaidia hata soko kuwa kubwa, ambapo mchimbaji ananufaika pia serikali itanufaika kupitia mapato hayo.

Alisema yapo ya madini ya aina mbalimbali na yapo maeneo mbalimbali, hivyo serikali iwaandae mazingira mazuri ya uchimbaji wanawake ili kuwaepusha na masuala ya ukatili wa kijinsia.

Aliongeza kuwa kuna machimbo yapo porini, hivyo inatakiwa miundombinu kwa wanawake iangaliwe upya.

Alisema elimu ikitolewa mara kwa mara itawasaidia wachimbaji kutorubuniwa na madalali wanaofika vijijini kununua madini hayo kwa bei ndogo.

Joyce Mkina kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) unaoratibu semina hizo, alisema kuwa Tanzania inatekeleza Sheria ya madini na kwamba ipo sheria ya mwaka 1867 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2007 na kuanza kutekelezwa mwaka 2010.

"Kutokana na sheria za madini, fursa zinatakiwa kupatikana katika madini ili kusaidia kuongezeka kwa mapato," alisema.

# Waziri Ummy aunda kamati kuchunguza mil. 700/- za bweni

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameunda kamati maalum kuchunguza matumizi ya Sh. milioni 700 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa bweni na bwalo la chakula katika Shule ya Sekondari ya Kumbukumbu ya Sokoine wilayani Mvomero, zinazodaiwa kutumika kinyume na maelekezo.

Aliyasema hayo jana wilayani Mvomero akiwa katika hitimisho la ziara yake ya kutembelea miradi ya maendeleo mkoani hapa.

Alisema serikali ilielekeza kiasi hicho cha fedha kwenye ujenzi wa bweni na bwalo kwenye shule hiyo, kwamba haitambui matumizi yaliyotumika katika kumalizia vyumba vya madarasa na jengo la utawala.

Hata hivyo, alisema matumizi ya fedha hiyo katika ukarabati huo hayaendani na hali halisi ya matumizi, kwamba aliiagiza kamati hiyo kutoka TAMISEMI kuchunguza suala hilo.

"Pamoja na matumizi mengi ya fedha hizo, mmebadilisha matumizi kwenye shule hiyo, lakini ujenzi haulingani na thamani halisi ya fedha iliyotolewa na matumizi hayo," alisema Ummy.

Hivyo, alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Hassan Njama, kutorudia tena kitendo cha kubadilisha matumizi ya fedha, huku akiwataka wakurugenzi wote nchini kujenga tabia ya kuandika maombi pale wanapotaka kubadilisha matumizi ya fedha zozote zinazowafikia hata kama wana mahitaji muhimu kwa wakati huo.

"Mkurugenzi wa halmashauri unapaswa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali kuu, wakati wa kutekeleza miradi, sababu kutofuata maelekezo kunaweza kukupeleka pabaya," alisema Ummy.

Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Mvomero, Hildegard Saganda, alisema fedha hizo zimebadilishwa matumizi kufuatia mwongozo wa Wizara ya Elimu kuwa shule inapaswa kufunguliwa, huku ikiwa imekamilika madarasa na kwamba wao walikuwa bado hawajakamilisha kwa mujibu wa mwongozo huo.

Akifafanua matumizi ya fedha hizo, Katibu Tawala Msaidizi wa Miundombinu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Ezron Kilamhama, alisema fedha hizo pia zilimegwa kiasi cha Sh. milioni 82 na kutumika katika ujenzi wa madarasa.

Alisema fedha iliyobaki wameitumia katika ujenzi wa bwalo na bweni zilivyoelekezwa awali, ujenzi ambao hata hivyo bado haujakamilika. Mradi wa Shule ya Sekondari ya Kumbukumbu ya Sokoine ujenzi wake ulianza mwaka 2010/2011 kumuenzi aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Edward Moringe Sokoine aliyefariki kwa ajali ya gari Aprili 12, 1984.



Baadhi ya wajasiriamalia wakisajili biashara zao katika banda la Brela kwenye maonyesho ya teknolojia ya uwekezaji katika sekta ya madini yanayofanyika mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwigulu: Nchi kwa sasa iko salama

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewataka Watanzania kutokuwa na wasiwasi, kwamba nchi kwa sasa iko salama.

Alitoa rai hiyo wakati akifunga Maonyesho ya Nne ya Teknolojia na Uwekezaji kwenye Sekta ya Madini, yaliyofanyika mkoani Geita.

Alisema Rais Samia Hassan yuko makini, anawapenda Watanzania, ana uzalendo na nchi yake na anafahamu tunapoelekea.

Nchemba alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwenda kwenye miradi ya maendeleo na kuwaomba Watanzania kusimamia fedha hizo kwa kushirikiana na viongozi.

Aidha, alisema lengo la maonyesho hayo ni muhimu kwa kuzingatia malengo ya mpango wa miaka mitano uliyobeba dhana ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, aliwapongeza wadau mbalimbali ambao wamejitolea kudhamini maonyesho hayo wakiongozwa na Kampuni ya GGML.

Alisema maonyesho hayo yametoa fursa ya kuelimisha umma juu ya fursa na huduma mbalimbali wanazotoa kwa jamii.

Makamu wa Rais anayeshughulika na miradi endelevu wa GGML, Simon Shayo, alisema GGML kwa miaka minne wamekuwa wadhamini wakuu kwenye maonyesho hayo.

Shayo alisema maonyesho hayo yanafungua fursa ya biashara na ukuaji kwa sekta ya madini.

"Tunaona wazi kwamba uwezeshaji wetu umechangia kwa namna moja au nyingine kudhihirisha kwamba sekta ya madini inaweza kuwa kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu," alisema Shayo.

Alisema Kampuni ya GGML imejitahidi kununua huduma za bidhaa hapa nchini tangu mwaka 2015, wameongeza huduma na bidhaa kwa zaidi ya asilimia 40.

# Ujerumani yapiga kura kuchagua wabunge, kansela

**Berlin, UJERUMANI**

WANANCHI wa Ujerumani wamepiga kura kulichagua bunge jipya, ambalo litatoa mwongozo wa atakayerithi kiti cha Kansela Angela Merkel, baada ya miaka 16 ya kuliongoza taifa lenye uchumi mkubwa kabisa barani Ulaya.

Mnyukano mkali katika uchaguzi huo, unahusisha kambi ya kihafidhina ya Kansela Merkel, inayohusisha vyama vya ndugu vya CDU/CSU, ambavyo mgombea wao ni Arimin Laschet na wa Chama cha Social Democrats-SPD, Olaf Scholz.

Watu milioni 60.4 kati ya raia wote milioni 83 wa Ujerumani ndio waliopiga kura kulichagua bunge, ambalo litakuwa na mamlaka ya kuchagua kiongozi mpya wa serikali.

Wajerumani wanachagua wabunge katika bunge la muungano huko Bundestag na kuna viti vipatavyo 598 na mara nyingi zaidi ya hapo.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa saa mbili asubuhi kwenye wilaya zote 299 za Ujerumani, ambako wapigakura watachagua Kansela mpya atakayeiongoza nchi katika makao makuu mjini Berlin.

Mgombea wa Chama cha SPD, Olaf Scholz, baada ya kupiga kura huko Aachen alitoa tamko.

Alisema kuna wapigakura walioamua kufika vituoni kupiga kura na kuna walioamua kupiga kura kwa njia ya barua, ikiwamo Kansela Angela Merkel kutokana na janga la virusi vya corona.

Kundi la muungano wa kihafidhina la Kansela Angela Merkel la CDU/CSU na chama cha wasoshalisti cha SPD, viko kwenye mchuano mkali vikikaribiana kabisa katika uchaguzi huu kumrithi.

Kura za maoni zinaonyesha kinyang'anyiro cha ukansela kinaweza kuleta matokeo kadhaa ikiwamo, muungano CDU-CSU kupata asilimia 23 kikitanguliwa kidogo na chama cha siasa za mrengo wa kushoto cha Social Democratic SPD kwa asilimia 25.

**DW**



Armin Laschet, anayegombea nafasi ya ukansela kutoka Chama cha Christian Democratic Union (CDU) ambaye ni Waziri Mkuu wa Jimbo lenye wakazi wengi zaidi Ujerumani, North Rhine-Westaphalia (NRW), akifurahi baada ya kupiga kura jana kuchagua wabunge katika Jiji la Aachen. **PICHA: AP**

# Daktari matatani kumchoma mkewe sindano ya sumu

**London, UINGEREZA**

DAKTARI kutoka Uingereza, raia wa Misri amepatikana na hatia baada ya kumdunga mke wake sindano ya sumu, alipokuwa katika harakati za 'kuyafukuza majini' yaliyokuwa yakimsumbua.

Mahakama ya Uingereza imeamua kumfunga kifungo cha miaka 14, kwa kumdunga sindano ya sumu aina ya Nicortin kwa lazima, kama njia ya kumtoa mashetani nyumbani kwao katika eno la Grimsby.

Mahakama ya Sheffield ilisikiliza ushahidi kuwa Metwally, mwenye umri wa miaka 34, akidai mke wake ana pepo wabaya.

Mahakama ilimpata na hatia ya makosa manane Metwally ikiwa ni pamoja na kudunga sindano yenye madhara pamoja na ulaghai.

Pia alipatikana na hatia ya kutazama picha za utupu, baada ya kupatikana na kamera za siri alizoziweka katika chumba cha mwanamke mmoja, ndani ya kliniki yake ya kibinafsi.

Kwa kipindi cha wiki nane, jopo la mahakama lilisikia ushahidi wa madai, ilisemekana aliamini kwamba kulikuwa na kiumbe au 'majini' ndani ya mwili wa mke wake na kwamba alikuwa akisoma aya kutoka ndani ya Qur'an na kumwaga maji ya mafuta kwenye mwili wa mpenzi wake Wilson.

Waraka wa mashtaka pia ulitaja kwamba mwanaume huyo alikuwa akishiriki katika aina 250 za matambiko pamoja na mpenzi wake na alirekodi makumi kadhaa ya video za matibabu hayo aliyoyaanza na mke wake tangu mwaka 2016.

Video 200 za tiba zilizorekodiwa, daktari Metwally, alisikika akimdunga mke wake kimiminika cha sumu ya Narcotin, huku akiwa amelala mbele yake bila fahamu kitandani.

Metwally, alikamatwa baada ya Wilson, Julai 4, mwaka 2019 alipokuwa mahututi na kulazimika kulazwa jioni baada ya kupoteza fahamu.

Jaji alisema kwamba Metwally huenda alikuwa anafikiria kuwa alikuwa akimsaidia, kwa njia iliyokatazwa na kwamba alifanya hivyo akitumia mchakato wa tiba usio na ufanisi na kumdunga na sumu kali za narcotic na kuhatarisha maisha yake.

**BBC**

## Japan, Uswisi, Hispania, K. Kusini, Singapore watu huishi zaidi duniani

NCHI tano duniani ikiwamo Japan, kutokana na utamaduni wake ikiwamo aina ya mlo, kunasababishi kuishi miaka mingi duniani ikilinganishwa na watu nchi zingine.

Wajapan huishi miaka 83 na kuwa miongoni mwa nchi zenye matarajio ya juu zaidi ya maisha marefu ya watu na kisiwa cha Okinawa, mara nyingi huitwa kisiwa cha wasiokufa, utafiti ulibaini zaidi ya watu 400 huishi hapo, wenye umri uliopita miaka miaka 100.

Wanasayansi walieleza kwamba hii inatokana na jinsi wenyeji wanavyokula, na hupendelea kula tofu kwa wingi iliyo na protini nyingi itokanayo na soya, viazi vitamu na samaki wachache.

Pia, ilibainika mazungumzo baina wazee na maisha ya kuishi pamoja, huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuishi maisha ya raha yasiyo na msongo wa mawazo.

Nchini Hispania, mafuta ya mzeituni, mboga na mvinyo ni mojawapo ya sababu za kuishi kwa umri mrefu miongoni mwa Wahispania, ambao wastani wa matarajio yao ya kuishi ni miaka 82.8.

Kupumzika mchana ni sababu nyingine na miji yake imeundwa kwa kuzingatia kutembea kwa miguu zaidi kuliko kuendesha magari.

Pia, nchini Singapore, mfumo wa afya unasababisha kila mkazi kupata huduma za afya na wastani wa matarajio ya muda wa kuishi ni miaka 83.1 na watafiti walieleza, nchi hiyo ina viwango vya chini vya vifo vya wanawake wakati wa kujifungua, kuliko nchi nyingine yoyote ile duniani ikijikita katika kuzuia badala ya kutibu magonjwa.

Pia, Uswisi, wanaume huishi miaka mingi kuliko nchi nyingine yoyote duniani, ikiwa na wastani wa miaka 81 ya kuishi.

Uswisi ni moja ya nchi tajiri zaidi duniani na barani Ulaya, hutoa hakikisho kwa wakazi wake la huduma za hali ya juu za afya, kiwango cha juu cha usalama wa mtu binafsi na maisha bora.

Baadhi ya utafiti hata ulionyesha maisha marefu ya Wanauswisi yanaweza kuhusishwa na ulaji jibini na bidhaa za maziwa, uchapakazi na kila upande ukizingatia haki ya watu ya kupata kufanya kazi na kucheza.

Katika Korea Kusini, ambayo ni nchi ya kwanza duniani kufikia wastani wa umri wa miaka 90 wa matarajio ya kuishi ya watu wake, kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni. Sababu ni zinatajwa uchumi imara na unaokua, upatikanaji wa huduma za afya kwa raia wake wengi na viwango vya chini vya shinikizo la damu, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani

Pia, mlo wa Wakorea huwa umejaa vyakula vilivyochachishwa ambavyo vinaaminiwa kushusha viwango vya mafuta mwilini na kuongeza kinga ya mwili na kuzuia saratani mbalimbali.

"Kwa ujumla, chakula cha Wakorea kina wanga mwingi utokanao na mimea na chenye virutubisho vya hali ya juu," alisema Camilla Hoheb, mwasisi na mwenyekiti wa taasisi ya utalii wa maisha bora duniani.

Heshima kwa wazee, kipaumbele kwa umma badala ya mtu binafsi na mahusiano, imara ya kijamii huwawezesha Wakorea kuimarisha viwango vya juu vya maisha bora.

**BBC**

# GINIKI, NATHALIA WALAMBA MAMILIONI NMB MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, Jumamosi aliongoza zaidi ya wakimbiaji 3,000 kushiriki mbio za Hisani za NMB Marathon 2021, ambazo Emmanuel Giniki na Nathalia Sule wa Arusha walitawazwa vinara wa kilomita 21 kwa wanaume na wanawake.

NMB Marathon 2021, zilizoanzia na kuishia viwanja vya Leaders Club chini ya kaulimbiu ya 'Mwendo wa Upendo,' ziliandaliwa na Benki ya NMB kwa kushirikiana na Hospitali ya CCBRT, zikilenga kukusanya fedha za kugharamia matibabu ya kinamama wenye maradhi ya fistula nchini.

Waziri Mkuu Majaliwa alishiriki mbio za kilomita tano, akiwaongoza viongozi kadhaa, wakiwamo Kamishna wa Idara ya Uhamiaji, Anna Makakala, Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Dorothy Gwajima, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amoss Makalla na Maofisa Watendaji Wakuu wa NMB na CCBRT, Ruth Zaipuna na Brenda Msangi.

Katika mbio hizo, Emmanuel Giniki wa Arusha aliibuka kinara kwa wanaume kilomita 21, akifuatiwa na Fabiano Sule wa Polisi Tanzania na Faraja Damas wa Jeshi la Wananchi, huku Nathalia Sule akifuatiwa na Secilia Ginoka wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Tunu Andrea wa Singida.

Kwa kuibuka vinara wa kilomita 21, Giniki alitwaa zawadi ya Sh. milioni 1.4, huku Fabiano akijinyakulia Sh. milioni 1.1 na Faraja akiambulia kiasi cha Sh. 700,000, zawadi sawa na walizotwaa washindi wa upande wa wanawake, Nathalia (wa kwanza), Secilia (wa pili) na Tunu (wa tatu).

Katika kinyang'anyiro cha Kilomita 10 Wanaume, Inyasi Sule kutoka Klabu ya Talent ya Arusha, aliibuka mshindi wa kwanza akifuatiwa na Mudrakat Ngachi JWTZ na Nelson Mbuya wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU), ambako Inyasi alijishindia Sh. 700,000, Mudrakat Sh. 500,000, na Mbuya akijipoza na Sh. 300,000.

Kwa upande wa wanawake Kilomita 10, Monalisa Leonard wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) alitawazwa mshindi akifuatiwa na Aisha Lubina wa Arusha, huku Rosalia Fabian wa JKU Zanzibar akimaliza nafasi ya tatu. Washindi hao wa upande wa wanawake, walijinyakukia zawadi sawa na walizoshinda wanaume, yaani pesa taslimu Sh. 700,000, Sh. 500,000 na Sh. 300,000.

John Slima aliibuka kinara wa mbio za kilomita tano wanaume akifuatiwa na Mkama Richard na Regan Allen, huku Hamida Nassoro akiongoza mbio hizo upande wa wanawake akifuatiwa na Suzana Thomas na Happiness Julius. Washindi hao wa kike na wa kiume, walijishindia Sh. 250,000, Sh. 150,000 na Sh. 100,000 kila mmoja.

Mtoto Mgima Saidi wa Dar es Salaam, aliibuka mshindi wa kilomita tano (wavulana), akifuatiwa na Ryan Nkusi na Abdallah Athumani (wote wa Dar), huku Lauren Dickson akiongoza mbio hizo upande wa wasichana, akifuatiwa kwa ukaribu na Vanessa Kabula na Rayyan Issa.



Wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania, wakijipongeza na medali zao baada ya kushiriki mbio za Hisani za NMB Marathon zilizokuwa na kauli mbiu 'Mwendo wa Upendo,' zikilenga kukusanya kiasi cha Sh. bilioni moja ili kufanikisha mpango wa matibabu ya fistula kwa kinamama wasio na uwezo nchini. Mbali na kushiriki mbio hizo zilizofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam, benki hiyo pia ilitoa mchango wa fedha kiasi cha Sh. milioni 10 kwa waandaaji wa mbio hizo ili kuunga mkono jitihada hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# Kapuya alia na umaliziaji Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI wa zamani wa wizara mbalimbali nchini ikiwamo iliyokuwa ya Habari, Utamaduni na Michezo (kwa sasa Sanaa, Utamaduni na Michezo), Juma Kapuya, amesema tatizo la Simba kwenye mechi ya Jumamosi dhidi ya Yanga lilikuwa ni umaliziaji.

Kapuya ambaye ni mwanachama wa klabu ya Simba, alisema timu yao haikucheza vibaya, lakini tatizo lilikuwa kwenye ushambuliaji, namna ya kuuweka mpira ndani ya wavu.

"Ukiangalia mpira tulikuwa tumewazidi kabisa, tatizo letu kubwa lilikuwa ni kufunga," alisema mbunge huyo wa zamani wa Urambo, baada ya mechi ya Ngao ya Jamii kumalizika na Simba kulala kwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Hata hivyo, pamoja na kupoteza mechi hiyo, Kapuya alisema ana imani na Simba kuutetea tena ubingwa wake msimu huu, na hata kufanya vema kwenye mechi za kimataifa.

"Kwenye ligi hatutofanya makosa tena kama haya, nadhani baada ya mechi hii viongozi watakaa kama kamati ya uongozi wajadili matokeo haya. Kwa hiyo nataka nikuhakikishie kuwa tutakaa sawa, tena kwa sababu tumefungwa tutakuwa makini zaidi," alisema.

Kapuya aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kuwapa muda wachezaji wapya ili wazoee mfumo na uchezaji wa klabu hiyo kama ilivyokuwa kwa Clatous Chama na Luis Miquissone.

"Wale walikuwa tayari wameshauzoea mfumo wa Simba, hawa bado kwa hiyo wakikaa na kuzoeana watakuwa wazuri," alisema.

Kapuya ni mmoja wa viongozi ambao hata walipokuwa wanashika nyadhifa mbalimbali serikalini kwenye wizara mbalimbali, hakuwa anaficha mapenzi yake kwa klabu hiyo kongwe nchini.

## U-20 wanawake yapiga mtu 3-0

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Soka Wanawake chini ya miaka 20, imeichapa Eritrea kwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Asmara nchini humo katika mechi, ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia kwa umri huo, ambayo fainali zake zinatafanyika mwakani nchini Costa Rica.

Akizungumza kutoka nchini humo jana, Kocha Mkuu Bakari Shime, alisema kwa sasa anaangalia mechi ya marudiano itakayochezwa Oktoba 9, mwaka huu nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), ni kwamba wachezaji walioanza kwa upande wa Tanzania ni Asha Mrisho, Christer Bahela, Fumukazi Nguruwe, Violeth Mwakamba, Enekia Kasonga, Joyce Lema, Emiliana Mdimu, Veronica Mapunda, Irene Kisisa, Aisha Masaka na Clara Luvanda.

Afrika itatoa timu mbili kwenda kwenye fainali hizo, nafasi ambazo ndizo zinashindaniwa kwenye michuano hiyo ya mtoano.

Ratiba inaonyesha mshindi kati ya timu ya Wanawake ya Tanzania U-20, atacheza na mshindi kati ya timu Burundi na Namibia, ambapo kwenye mechi ya kwanza, Burundi ikiwa nyumbani ilishinda mabao 3-0.

## ZFF kutoa darasa usajili wa mtandao

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limejipanga kutoa elimu kwa klabu zote za Zanzibar kuhusu matumizi ya mfumo wa usajili kwa msimu huu wa 2021/22.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema kuelekea msimu mpya klabu zote zinatakiwa kutumia mfumo wa mtandao kwenye usajili na uhamisho.

Alisema katika msimu uliopita matumizi ya mfumo huo ambao ndio kwanza ulianzishwa ni klabu madaraja machache yalifanikiwa kuutumia ambayo ni klabu za Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja pamoja na Klabu za Ligi Daraja la Mkoa wa Mjini Magharibi pekee.

Alisema msimu huu klabu za ligi zote za Zanzibar tayari vimeingizwa katika mfumo huo na usajili na kinachoendelea kwa sasa ni mchakato wa kutoa elimu ya namna ya kufanya usajili na uhamisho wa wachezaji kwa njia ya mfumo huo katika kipindi hiki cha dirisha la usajili.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JUVE KUMUUZA RAMSEY
JUVENTUS inajiandaa kumuuza kiungo wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30 katika dirisha la usajili la Januari - huku West Ham, Everton na Newcastle zikihusishwa naye. **(Sun)**

### INTER YAMTAKA LENO
INTER Milan inawania kumsajili golikipa wa Arsenal na Ujerumani, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 29, katika orodha yao. **(Fichajes)**

### KULUSEVSKI AWANIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur, inafikiria kumsajili kiungo wa Juventus na Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 21. **(Mirror)**

### CHELSEA KUMUUZA KANTE
CHELSEA ipo tayari kumuuza kiungo wake, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 30 kipindi cha majira ya joto kijacho. **(Fichajes)**

### SAYUNCU ATAKIWA MADRID
MLINZI wa Leicester City na Uturuki, Caglar Soyuncu mwenye umri wa miaka 25, anawaniwa na Real Madrid**. (DefensaCentral)**

### DAMSGAARD KWA SPURS, JUVE
KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili winga wa Sampdoria na Denmark, Mikkel Damsgaard mwenye umri wa miaka 21, huku pia akiwaniwa na Juventus. **(Tuttosport)**

### EN-NESYRI KUIGHARIMU ARSENAL
ARSENAL watatakiwa kulipa pauni milioni 38.5 kama wanataka kumsajili straika wa Sevilla, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 24. **(Mundo Deportivo)**

### CHIESA AWANIWA DARAJANI
CHELSEA inajiandaa kutoa ofa kwa winga wa Italia, Federico Chiesa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Juventus akitokea Fiorentina. (**Calciomercato)**

### MUKIELE KUTUA MAN UNITED
MANCHESTER United inaangalia uwezekano wa kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Ufaransa, Nordi Mukiele mwenye umri wa miaka 23. **(Fihajes)**

### WERNER NUSURU ATUE MAN
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, alitaka kujiunga na Manchester United kabla ya kutua kule Stamford Bridge. **(Bild)**

### WEST HAM YAMTAKA BAYO
WEST Ham inataka kumsajili straika wa Clermont na Guinea, Mohamed Bayo mwenye umri wa miaka 23. **(Sun)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES AOMBA RADHI KUKOSA PENALTI

●●● Hakuna mtu aliyechanganyikiwa na kujisikia vibaya kama mimi kwa kukosa na matokeo yake kufungwa...

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Bruno Fernandes ameomba radhi baada ya kukosa penalti dakika za majeruhi wakati timu yake ikikumbana na kipigo kutoka kwa Aston Villa kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

United walishtukizwa kwa kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Villa hao kwenye dimba la Old Trafford Jumamosi, na Fernandes akaipaisha penalti yake.

Nyota wa Villa, Kortney Hause ndiye aliibuka shujaa kwenye mchezo huo huku akifunga dakika ya 88 na dakika tano baadaye kusababisha penalti.

Hata hivyo, Fernandes alichukua jukumu la kupiga penalti hiyo mbele ya nyota mwanzake, Cristiano Ronaldo na kuipaisha juu ya goli na United ikafungwa mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu na ikafikisha jumla ya mechi nne ilizopoteza kwenye mashindano yote msimu huu.

Fernandes alikosa penalti hiyo kwa mara ya kwanza kati ya 23 alizopiga hapo United kwenye mashindano yote na mara ya kwanza tangu Oktoba 2020 dhidi ya Newcastle United kwenye Ligi Kuu.

"Hakuna mtu aliyechanganyikiwa na kujisikia vibaya kama mimi kwa kukosa penalti na matokeo yake tumefungwa," alisema Fernandes akiandika kupitia mitandao ya kijamii.

"Mara zote napenda kutimiza majukumu yangu na kukumbatia presha niliyonayo kama kwenye nyakati kama hizi.


"Leo (juzi), nilishindwa. Lakini naangalia hatua mbele zaidi kwa ajili ya changamoto mpya kwa ari ileile ya kutekeleza majukumu yangu.

"Katika matukio mengi, mpira unakuwa tofauti na kupoteza sio jambo zuri sana kwetu.

"Kuna kuwa na shutuma nyingi na hii ni sehemu ya mpira wa miguu. Nimejifunza mengi katika kuhakikisha kwamba nakubaliana na hali halisi."

MECHI KALI
HOME
AWAY
CRYSTAL PALACE
3.02 | 3.12 | 2.48
BRIGHTON
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# GUARDIOLA AWEKA REKODI MAN CITY

**LONDON, England**

PEP Guardiola anajisikia fahari kuweka rekodi ya kuwa kocha aliyeshinda mechi nyingi zaidi na Manchester City wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Kocha huyo kutoka Catalunya alifikisha mechi ya 221 alizoshinda tangu alipowasili hapo City mwaka 2013, akiipiku rekodi iliyowekwa na kocha, Les McDowall.

City ilipata ushindi huo kwenye dimba la Stamford Bridge, bao pekee likifungwa na Gabriel Jesus, na kufikisha pointi sawa na Chelsea.

Guardiola alifungwa mechi tatu na Chelsea, zote chini ya kocha Thomas Tuchel, ikiwamo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa jijini Porto, Mei mwaka huu.

"Vijana walikuwa bora leo (juzi)," alisema Guardiola akiiambia BT Sport.

"Katika uwanja huu, dhidi ya mpizani wetu, kufanya kile tulichokifanya kinanifanya mimi nijisikie fahari.

"Tulikuja hapa kucheza mchezo wetu. Wakati mwingine huwezi kufanya hivyo. Tulicheza kwenye kiwango bora na tungeweza kuwa bora zaidi."

# Conte azikataa Arsenal, Barca

**LONDON, England**

KOCHA Antonio Conte hana mpango wa kujiunga na Barcelona ama Arsenal kwa muda huu kwa kuwa anataka kuanza na timu tangu mwanzo wa msimu, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Conte mwenye umri wa miaka 52, kwa sasa hana kazi kutokana na kuvunja mkataba na Inter Milan baada ya kuwaongoza kutwaa ubingwa wao wa kwanza wa Serie A baada ya kuukosa miaka 10.

Kama sehemu ya makubaliano ya kuvunja mkataba, Conte amezuiwa kujiunga na timu nyingine ya Seria A mpaka msimu mpya unaofuata na si sasa.



Ripoti zimeeleza kuwa Conte alikuwa amewekwa kwenye rada za Barcelona na Arsenal ila amekacha madili hayo na badala yake anataka kuanza na timu tangu mwanzo.

Arsenal ambayo inanolewa na kocha, Mikel Arteta hayupo kwenye kiwango bora msimu huu, huku Barcelona nao wakipambana kurudi kwenye kiwango chao.

## HABARI MICHEZO


LIVE IN PLAY

BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP

CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA



PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 27 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3177 | Seoul E Land vs Busan I Park | 2.27 | 3.18 | 2.94 |
| 14:00 | 1593 | Astana vs Taraz | 1.38 | 4.47 | 6.81 |
| 15:00 | 3023 | Ipswich U23 vs Bristol City U23 | 4.36 | 3.82 | 1.66 |
| 15:00 | 3980 | Coventry U23 vs Sheffield Wednesday U23 | 1.47 | 4.46 | 5.23 |
| 15:00 | 5136 | Cardiff City U23 vs Millwall U23 | 1.59 | 3.96 | 4.64 |
| 15:30 | 3527 | Birmingham U23 vs Southampton U23 | 1.67 | 4.20 | 4.40 |
| 16:00 | 1267 | Fiorentina Youth vs Sassuolo Youth | 2.38 | 3.59 | 2.52 |
| 16:00 | 1879 | Sampdoria Youth vs Bologna Youth | 1.46 | 4.55 | 5.23 |
| 17:00 | 1063 | Ural Yekaterinburg vs Arsenal Tula | 2.44 | 3.16 | 2.87 |
| 17:00 | 2689 | Lokomotiv Tashkent vs Mash AL Mubarek | 1.47 | 3.96 | 6.18 |
| 17:00 | 5948 | Nasaf Qarshi vs Bunyodkor | 2.03 | 3.40 | 3.70 |
| 17:15 | 1766 | PAS Giannina vs OFI Crete | 2.47 | 3.01 | 2.96 |
| 17:30 | 4301 | Pirin Blagoevgrad vs Cherno More | 3.05 | 3.29 | 2.16 |
| 18:00 | 2343 | Napoli Youth vs Pescara Youth | 1.93 | 3.73 | 3.25 |
| 18:00 | 5013 | Gaz Metan Medias vs Sepsi Osk | 3.94 | 3.15 | 1.97 |
| 19:00 | 1430 | Proleter vs FK Napredak | 2.43 | 3.49 | 2.52 |
| 19:00 | 4378 | GKS Piast Gliwice vs Cracovia | 2.00 | 3.18 | 3.57 |
| 19:00 | 5227 | Hrvatski Dragovoljac vs Istra | 3.77 | 3.58 | 1.82 |
| 19:00 | 5618 | Ararat Yerevan vs Pyunik Yerevan | 1.97 | 3.48 | 3.33 |
| 19:00 | 5878 | Nizhny Novgorod vs CSKA Moscow | 4.63 | 3.55 | 1.73 |
| 19:30 | 1259 | Atromitos vs Aris Salonica | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 19:30 | 2666 | Chernomorets Odessa vs FC Ingulets | 2.61 | 3.19 | 2.51 |
| 19:30 | 2963 | Chateauroux vs Sedan | 1.93 | 3.23 | 3.91 |
| 19:30 | 5916 | Apollon Smyrnis vs Ionikos Nikea FC | 2.39 | 3.05 | 3.05 |
| 19:45 | 2893 | Lokomotive Sofia vs Slavia Sofia | 2.41 | 3.04 | 2.85 |
| 20:00 | 1143 | Wolverhampton U23 vs Sunderland U23 | 1.80 | 3.78 | 3.63 |
| 20:00 | 2188 | Trabzonspor vs Alanyaspor | 1.58 | 4.15 | 4.94 |
| 20:00 | 2344 | IFK Goteborg vs Kalmar | 2.61 | 3.04 | 2.61 |
| 20:00 | 2529 | Kasimpasa vs Konyaspor | 2.51 | 3.20 | 2.75 |
| 20:00 | 3296 | Degerfors vs AIK Football | 4.65 | 3.58 | 1.67 |
| 20:00 | 3804 | Apoel Nicosia vs Paeek | 1.23 | 5.72 | 11.84 |
| 20:00 | 3945 | Halmstads BK vs Sirius FK | 2.05 | 3.15 | 3.44 |
| 20:00 | 4255 | Denizlispor vs Samsunspor | 6.61 | 4.28 | 1.41 |
| 20:00 | 4946 | Aarhus vs Sonderjyske | 1.76 | 3.64 | 4.32 |
| 21:00 | 1390 | Burnley U23 vs Reading U23 | 1.80 | 3.78 | 3.63 |
| 21:00 | 1544 | Tottenham U23 vs Derby County U23 | 1.97 | 3.90 | 3.35 |
| 21:00 | 1616 | Universitatea Craiova vs Dinamo Bucuresti | 1.36 | 4.52 | 8.25 |
| 21:00 | 1980 | Pacos Ferreira vs Belenenses | 1.70 | 3.44 | 5.11 |
| 21:00 | 2655 | Jong Ajax vs Maastricht | 1.59 | 4.29 | 4.49 |
| 21:00 | 4586 | Norwich U23 vs West Bromwich U23 | 2.60 | 3.80 | 2.42 |
| 21:00 | 4850 | Cukaricki St vs Radnik Surduluca | 1.43 | 4.26 | 6.19 |
| 21:00 | 5924 | Stoke City U23 vs Aston Villa U23 | 1.89 | 3.71 | 3.37 |
| 21:45 | 1477 | Toulouse vs Caen | 1.53 | 3.94 | 5.90 |
| 21:45 | 2832 | Dundalk FC vs Bohemians FC | 2.36 | 3.29 | 2.71 |
| 21:45 | 4138 | Venezia vs Torino | 3.52 | 3.42 | 2.09 |
| 22:00 | 2561 | Catanzaro vs Catania | 1.84 | 3.37 | 4.35 |
| 22:00 | 3184 | Fuenlabrada vs FC Cartagena | 2.04 | 2.96 | 4.04 |
| 22:00 | 4014 | Celta Vigo vs Granada | 1.65 | 3.91 | 5.22 |
| 22:00 | 4334 | Crystal Palace vs Brighton | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 23:15 | 4149 | Boavista vs GD Estoril | 2.66 | 2.96 | 2.76 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MARTINEZ AZUNGUMZIA KUWA KOCHA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

ROBERTO Martinez amesema hana la kusema baada ya kuhusishwa kwake na kazi ya kuinoa Barcelona.

Bosi wa sasa wa Barca, Ronald Koeman anaendelea kwa chini ya shinikizo kubwa wakati timu hiyo ikionekana kuwa na kiwango kibovu zaidi.

Barcelona walichapwa mabao 3-0 na Bayern Munich wakiwa nyumbani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na pia walikuwa na kipengele kwenye LaLiga, wakitoa sare ya bao 1-1 na Granada.

Matokeo hayo mawili yamezidisha shinikizo kwa Koeman, ingawa haionekani kuwa Mholanzi huyo atafutwa kazi katika siku za hivi karibuni.

Martinez mara nyingi amekuwa akihusishwa na kuchukua nafasi ya ukocha pale kwenye dimba la Camp Nou.

Alipoulizwa juu ya matarajio ya kuchukua kibarua hicho, bosi huyu wa zamani wa Everton na Swansea hakuwa na la kusema.

"Kama unavyofikiria, hakuna chochote kwa kweli, hakuna chochote ambacho ninaweza kuzungumzia," alisema Martinez akinukuliwa na Marca.

"Ni wazi, kuwa ni kawaida kuwa na uvumi kila wakati, hili lipo kila wakati. Hii ni kawaida katika soka.

"Unapopoteza michezo mitatu, uvumi unasema kwamba utapoteza kazi yako. Lakini sina maoni ya kusema juu yangu kwa wakati huu."



# Martial mbadala wa Haaland

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial endapo watamuuza straika wao, Erling Haaland katika majira yajayo ya kiangazi.

Mkataba wa Haaland wa sasa unakipengele ambacho kitamfanya kuuzwa kwa bei ya euro milioni 75 kuanzia majira ya kiangazi mwaka 2022.

Martial anaangaliwa kama mbadala mzuri wa mshambuliaji huyo baada ya kukosa namba katika kikosi cha kwanza cha Ole Gunnar Solskjaer hasa baada ya kurejea kwa mshambuliaji wao wa zamani Cristiano Ronaldo.

Martial amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake wa sasa ambao unatarajiwa kukamilika Juni mwaka 2024.

Dortmund wanaweza kuwashawishi United kumuuza mchezaji huyo endapo watatoa dau zuri kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo.

# Michezo

Jumatatu Septemba 27, 2021

Nipashe



**Fernandes aomba radhi kukosa penalti** UKURASA 21

**NMB MARATHON...**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, wakifanya mazoezi baada ya kukimbia mbio za kilomita tano za NMB Marathon zilizofanyika mwishoni mwa wiki katika viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam. **HABARI UK. 20**

# MTIFUANO SIMBA, YANGA SASA WAHAMIA LIGI KUU

## Azam FC, Coastal Union, Mtibwa kuanza mbio za ubingwa leo, huku watani hao wenyewe wakishuka...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Yanga kuionyesha ubabe Simba katika mechi ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2021/22, kwa kuitandika bao 1-0 kwenye mechi ya Ngao ya Jamii, mbio za kuwani ubingwa wa ligi hiyo msimu huu sasa zitaanza rasmi leo kwa kupigwa mechi tatu katika viwanja tofauti nchini.

Juzi, Jumamosi miamba hiyo ilikutana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, na Yanga kufanikiwa kubeba Ngao ya Jamii, shukrani zikimwendea Fiston Mayele aliyeizamisha Simba kwa bao hilo pekee katika dakika ya 13.

Ligi hiyo sasa itaanza leo kwa Mtibwa Sugar kuikaribisha Mbeya Kwanza FC katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, wakati Namungo FC ikiwa mwenyeji wa Geita Gold FC katika Dimba la Ilulu mkoani Lindi na Azam FC ikikabiliana na Coastal Union ugenini katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Mabingwa watetezi, Simba wataanza kampeni yake ya kuwania kutwaa taji hilo kwa mara ya tano mfululizo wakiwa ugenini kesho dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Mchezo mwingine utakaopigwa kesho utakuwa kati ya Dodoma Jiji ambayo itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati Mbeya City ikiwa mwenyeji wa Tanzania Prisons katika dimba la Sokoine jijini Mbeya.

Wababe wa Simba kwenye Ngao ya Jamii, Yanga, wenyewe watashuka Dimba la Kaitaba mjini Bukoba keshokutwa, Jumatano kuwavaa wenyeji wao, Kagera Sugar, hiyo ikiwa ni moja kati ya mechi mbili zitakazokamilisha michezo ya kwanza ya raundi hiyo ya kwanza kwa kila timu. Mechi nyingine itayopigwa keshokutwa ni Polisi Tanzania FC ikiikaribisha KMC FC katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi

Kuelekea mechi za leo, Coastal Union imejigamba kuendeleza ubabe mbele ya Azam FC katika Uwanja wa Mkwakwani, lakini 'Wanalambalamba' hao nao hawakuwa kimya kujibu mapigo.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Melis Medo, akizungumzia mechi hiyo jana, aliiambia Nipashe kuwa amejiandaa vizuri kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

Alisema anawaheshimu Azam FC ni timu nzuri na wao pia wako vizuri na tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri kwa mchezo huo kupata pointi muhimu.

"Tuko tayari kukabiliana na Azam FC, kila kitu kinaenda vizuri na wachezaji wangu wako fiti kupambana na kuendelea kutumia vema uwanja wetu wa nyumbani," alisema Medo.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wamefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kwenda kupata matokeo ugenini dhidi ya Coastal Union.

Alisema baada ya kumaliza mechi ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, wachezaji walipewa mapumziko mafupi na wamerejea kwa ajili ya kuendelea na mapambano ya msimu mpya wa ligi hiyo.

"Ligi itakuwa ngumu, timu nyingi zimejiandaa kuanzia usajili hata maboresho ya benchi la ufundi, tuko vizuri kwenye maandalizi yetu msimu huu kutafuta matokeo mazuri kwa kila mechi iwe ugenini ama nyumbani," alisema kocha huyo.

Kwa misimu mitatu, Azam FC hawajawahi kupata ushindi katika Uwanja wa Mkwakwani, baada ya msimu wa 2018/19, Februari 19 kuambulia sare ya bao bao 1-1, kisha Desemba 29 msimu wa 2019/20 kuchapwa bao 1-0 na msimu uliopita Februari 11, mwaka huu kulambwa mabao 2-1.

# Nabi, Gomes wafunguka

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewapongeza wachezaji wake kwa kuibuka na ushindi dhidi ya Simba kwenye Ngao ya Jamii juzi, huku akisema sasa amepanga kufanya mambo mawili kwa pamoja ndani ya kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania, unaoanza leo kabla ya kikosi chake kushuka dimbani keshokutwa, Jumatano.

Nabi ameyasema hayo baada ya kikosi chake kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Simba na kutwaa taji la Ngao ya Jamii juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha huyo mbali na kuwapongeza wapinzani wao kwa kucheza vizuri, lakini aliwasifu wachezaji wake kwa kufuata maelekezo aliyowapa ya kutafuta bao la mapema na kulilinda.

Alisema sasa wanapambana kuhakikisha wanashinda mechi zao zote za ligi hiyo pamoja na kuhakikisha anaendelea kupata muunganiko wa wachezaji wake kwa asilimia 100.

"Bado nahitaji muda wa kutengeneza muunganiko kwa wachezaji wangu, huku tukipambana kutafuta matokeo katika mechi za ligi pia nitazitumia kwa ajili ya kuimarisha kikosi changu," alisema.

Naye muuaji wa Simba, Fiston Mayele, alisema: "Simba wako vizuri, matokeo haya hayatufanyi kujiona bora, tunaendelea na maandalizi kwa ajili ya ligi, katika mchezo wetu wa Jumatano dhidi ya Kagera Sugar."

Wakati wakisema hayo, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa na wachezaji wake walipambana kutafuta matokeo, lakini bahati haikuwa yao.

"Wachezaji wamepambana sana kutafuta matokeo, haikuwa bahati yetu, kuhusu nafasi ya Clatous Chama na Luis Miquissoine, tayari zimepatiwa watu ambao wanahitaji muda wa kuzoeana na kutengeneza kombinesheni," alisema Gomes.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >